epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Januari 30, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • Na. 0581937
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ

UKURASA WA 2
**Ndumbaro:** Kampeni ya Samia haitawaacha salama wakiukaji wa haki za binadamu



UKURASA WA 3
**Donge** nono la kustaafu CAG, Katibu Mkuu Kiongozi laja

UKURASA WA 11
**Hadhi** Maalum kwa Diaspora yachomolewa tena bungeni



UKURASA WA 21
VINICIUS JR AANDALIWA DAU NONO SAUDIA

# Hali tete DRC

• **Samia** aongoza kikao cha dharura SADC, maiti zatapakaa, balozi zashambuliwa, Marekani yawaondoa watu wake... *Endelea Ukurasa 19*



Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC-Organ), Rais Samia Suluhu Hassan akiongoza Mkutano wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Asasi hiyo, Ikulu jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: IKULU**

MKUTANO NISHATI

## Namna Tanzania ilivyovuna, siku mbili Dar katika sura mpya

UKURASA 18



# Lissu ataka Bunge la dharura kufumua sheria za uchaguzi

• **Wakuu** CHADEMA kujifungia wiki nzima; watoa mbinu kukabili uamuzi wa Trump... *Endelea Ukurasa 2*

**MICHEZO** AZIK KI, MZIZE RASMI SOKONI UK.24
**KATUNI** UK.6



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro (wa tatu kushoto), akipata maelezo kabla ya kuzindua Kampeni ya Msaada wa Sheria ya Mama Samia, mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Lissu ataka Bunge la dharura kufumua sheria za uchaguzi

**Na Halfani Chusi**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu ameshauri serikali kuitisha Bunge la dharura kufanya marekebisho ya sheria za uchaguzi, akisisitiza msimamo wa chama hicho wa 'hakuna uchaguzi bila mabadiliko'.

Vilevile, chama hicho kimetoa mapendekezo matatu kwa serikali kukabili mabadiliko ya kisera kwenye misaada katika sekta ya afya yaliyofanywa na Rais wa Marekani, Donald Trump.

Lissu alisisitiza msimamo huo jana mkoani Dar es Salaam muda mfupi baada ya kukabidhiwa rasmi ofisi katika makao makuu ya chama hicho, Mikocheni, wilayani Kinondoni.

Lissu alisema kuna Uchaguzi Mkuu Oktoba mwaka huu, lakini kwao CHADEMA, kama hakuna mabadiliko, hakuna uchaguzi. Lakini haina maana watasusia uchaguzi.

"Tusijaribu kuitanua lugha kuliko maana yake ya kawaida, hakuna mabadiliko, hakuna uchaguzi. Lazima tuzungumze hayo mambo mawili tuone tunawezaje tukaenda nayo mbele aidha kwa pamoja au kuamua lipi muhimu.

"Sasa hilo sitaki nizungumze hapa, zaidi tunakwenda kujifungia kisha tutaamua kwa pamoja ili uwe uamuzi wa chama na si wangu peke yangu. Tutakwenda kuonana na marafiki zetu duniani tuwaambie msimamo wetu hadharani. Tutawaomba watuunge mkono, na wale wasiotupenda tutawaangalia usoni, tutawaambia msimamo wetu ni huu," Lissu alisema.

Mtaalam huyo wa sheria alisisitiza msimamo huo wa 'no reforms no election' siyo wake, bali ni wa chama na kwamba kazi yake ni kutekeleza maagizo ya chama.

Kwa mujibu wa Lissu, chama hicho hakiwezi kwenda kwenye uchaguzi ambao alisisitiza kuwa kuingia katika uchaguzi kwa hali ya sasa ni kukubali kunyolewa au kuwa kama kondoo anayepelekwa machinjioni.

"Tunazungumzia kupata mageuzi kwa shuruti kama walivyopata Kenya, Malawi, Bunge letu linaweza kukaa muda wowote hata bila kuwa na ratiba," alisema Lissu

Alikumbushia kipindi cha nyuma Bunge liliwahi kuitishwa kwa dharura siku ya Jumamosi kuidhinisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar katika ukumbi wa Karimjee, na Muungano mpaka leo upo, hivyo kwa suala la katiba haiwezi kuwa ajabu.

Lissu pia alisema wafuasi wote wa chama hicho watakuwa na haki sawa kulingana na uwezo na kukitumikia chama, na kwamba waliokuwa timu Lissu wasitarajie upendeleo na timu Mbowe kuumizwa, bali wote watakuwa na haki sawa.

Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, John Heche alisema wamejipanga kufanya kazi kikamilifu huku wakilitaka Jeshi la Polisi kuacha kuwatishia kwa kuwa wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika alisema chama hicho chini ya viongozi wapya na wastaafu, watajifungia ndani kwa muda wa wiki moja kwa ajili ya kuja na mkakati wa pamoja kuelekea uchaguzi.

Kuhusu aliyekuwa Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe kutoonekana wakati wa makabidhiano ya ofisi, Mnyika alisema katiba ya chama hicho inaruhusu Katibu Mkuu kusimamia zoezi hilo na kwamba hakuna shida kama watu wanavyodhani.

#### SERA ZA TRUMP

Wakati huo, CHADEMA imetoa mapendekezo matatu kwa serikali kufuatia uamuzi wa Rais wa Marekani, Donald Trump kusitisha misaada kwa sekta ya afya.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Afya na Maendeleo ya Jamii ya Bunge la Wananchi CHADEMA, Ashura Masoud, lazima hatua zichukuliwe kukabili mabadiliko hayo.

Chama hicho kimependekeza serikali kuandaa mkakati wa dharura wa kisera na kibajeti wa kuhakikisha inakuwa na fedha za kutosha kwenye Mfuko wa Kudhibiti UKIMWI na Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI kwa kubana matumizi na kutenga vyanzo maalum na vya lazima katika bajeti ya taifa, ili kupunguza makali ya uhaba wa fedha za ARV na UKIMWI.

Pia Bunge linaloendelea sasa kujadili ajenda ya dharura, serikali iwasilishe taarifa ya tathmini na mkakati wa kina wa namna ya kukabiliana na upungufu wa fedha katika sekta ya afya na nyingine za maendeleo kisha litokea na azimio.

"Rais Samia Suluhu Hassan na wakuu wenzake wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Umoja wa Afrika (AU) wafanye mkutano kwa ajili ya kutafuta ufumbuzi mpana na wa kina zaidi kupata vyanzo mbadala vya fedha na kuziba pengo la kibajeti linalosababishwa na Marekani kusitisha misaada ya maendeleo," alishauri.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa asilimia 90 ya fedha zinazotumika katika eneo hilo ni kutoka nje ambapo Mpango wa Dunia wa Rais wa Marekani wa kukabiliana na UKIMWI (PEPFAR) unachangia asilimia 40 katika kapu hilo na michango ya mashirika mengine kama WHO, Kituo cha Kudhibiti Magonjwa cha Marekani (CDC) na Global Fund.

"Idadi ya waathirka wa VVU hadi sasa wanaonufaika na misaada ni takribani milioni 1.5, na wastani wa Sh. bilioni 204 kwa mwezi hutumika," alisema.

Nipashe ilimtafuta Waziri wa Afya, Jenista Mhagama, ambaye kupitia msaidizi wake, alisema suala hilo litatolewa ufafanuzi baada ya kuzungumza na wakubwa wa nchi kisha kutolewa taarifa kwa umma na si mwandishi mmoja mmoja.

***Kwa maoni; +255 677 020 701 Email; costumerrelations@guardian.co.tz***

# 'Kampeni ya Samia haitawaacha salama wakiukaji wa haki'

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, amesema Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia itapita kila halmashauri, wilaya, kata, vijiji na vitongoji na mitaa yote kuhakikisha kila mtanzania ananufaika na huduma hiyo bila malipo.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza kwenye uzinduzi wa kampeni hiyo kwa mkoa wa Kilimanjaro, viongozi mbalimbali wakishiriki uzinduzi huo.

"Kwenye kampeni hii, hakuna jiwe litakaloachwa bila kuguswa. Kila mgogoro utatatuliwa. Tuna awamu ya kwanza na ya pili, hivyo kila Mtanzania mwenye mgogoro wake ataguswa na wale waliozoea kukiuka haki za watu, hatutawaacha salama, maana tutapita kila kona.

"Katika mikoa 16 tuliyopita, tumeona wananchi wengi wana kiu ya haki na ndiyo maana wamekuwa wanajitokeza kwenye kampeni na sisi tunawatimizia mahitaji yao, Haya ni maono na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyeona kiu ya haki ya watanzania," alisema.

Dk. Ndumbaro alisema kampeni hiyo yenye maudhui ya kusaidia wananchi, ina mambo 10 na itapita kila eneo la Tanzania Bara na Visiwani.

"Katika kampeni hii kila kichaka kitakatwa na kuchomwa moto, kuna watu wanajificha kwenye vichaka vya ukatili tutavikata ili haki itendeke. Mama Samia Legal Aid ni ibada kwa sababu inatenda jambo jema lililoandikwa na maandiko yote.

"Tutahakikisha Mama Samia Legal Aid inaleta haki itakayoinua taifa la Tanzania, kampeni hii ni jambo la kikatiba na sheria na imekuja na falsafa ya 'Gusa Achia Twende na Mama Samia Legal Aid' na pia imekuja na falsafa ya 'Ubaya Ubwela' kwa wanaokiuka haki za binadamu, wanaokiuka sheria, wanaofanya ukatili wa kijinsia tutawanyoosha," alisema.

Rais wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), Boniface Mwabukusi, alisema huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi ni kama ibada, hivyo ni wajibu wa wanaotoa huduma hiyo kuifanya kwa unyenyekevu na kwa ukamilifu.

Alisema migogoro mingi iko kwenye mirathi na ardhi na kwamba hayo yote yanachangiwa na watu kuogopa kuandika wosia, hali ambayo imekuwa inachochea migogoro baada ya mhusika kufariki dunia.

"TLS section IV inataja huduma hii ya msaada wa sheria na tunaipa huduma hii kipaumbele kikubwa sana kusukuma huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi. Tutaunga mkono serikali kuwasaidia wananchi wengi wenye shida wapate haki," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdini Babu alipongeza kampeni hiyo kupelekwa mkoani mwake, akidokeza kuwa wapo wananchi wengi wenye changamoto ya migogoro ya kisheria, lakini hawajui sehemu ya kwenda kupata haki.

"Tuna madawati ya msaada wa sheria kwenye ofisi mbalimbali hapa mkoani, lakini baada ya kuzindua leo (jana) hapa tutakwenda kwenye kata zote ambako kuna wananchi wengi wenye changamoto ya kupata haki. Kwa hiyo kampeni hii ni mwafaka," alisema.

Mwakilishi wa Chama cha Mawakili wa Serikali, Yohana Marko, alisema mawakili wa serikali wana wajibu wa kisheria wa kutoa elimu ya msaada wa kisheria huku akiahidi kuwa chama kitatekeleza kwa nguvu zote suala la msaada kwa kufuata mwongozo wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Alisema hiyo itakuwa ajenda ya kudumu ndani ya Chama cha Mawakili wa Serikali na uongozi wa chama utahakikisha wananchi wanaendelea kunufaika na huduma za msaada wa sheria.

Mbunge wa Moshi Mjini (CCM), Jacob Tarimo alisema watu wengi wamekuwa wanafika ofisini kwake kuomba msaada wa sheria, hivyo ujio wa kampeni hiyo ni ukombozi kwao.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Amon Mpanju alimpongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Ndumbaro, kwa kufanikisha huduma hiyo ya msaada wa sheria kwa wananchi wasio na uwezo kupata haki zao.

***Imeandaliwa na Godfrey Mushi na Joseph Mwendapole***

# Donge nono la kustaafu CAG na Katibu Mkuu Kiongozi laja

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limepitisha marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298, kwa kuongeza maslahi manono kwa Katibu Mkuu Kiongozi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) pindi wanapostaafu kutokana na nafasi zao kuwa nyeti na wanazitumikia kwa uzalendo na uadilifu.

Katika marekebisho hayo, mafao ya Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu kama mkuu wa utumishi wa umma yameboreshwa, huku Rais akipewa mamlaka ya kuamua au kurekebisha mshahara, marupurupu na manufaa mengine ya CAG wakati akiwa kazini, anapostaafu, anapoondolewa kazini au anapojiuzulu.

Akiwasilisha bungeni jana Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa Mwaka 2024, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari alisema kuwa mbali na manufaa yanayotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma, Katibu Mkuu Kiongozi atapewa na mamlaka husika mafao ya kustaafu.

Alisema serikali ilipendekeza Katibu Mkuu mstaafu kupewa hati ya kusafiria ya kidiplomasia kwa ajili yake na mkewe, matibabu kwa ajili yake na mkewe yatakayogharamiwa na serikali ndani ya Jamhuri ya Muungano au nje ya Jamhuri ya Muungano baada ya rufani kutoka Hospitali ya Taifa.

Pia alisema huduma ya gari moja litakalotolewa na serikali na kubadilishwa kila baada ya miaka saba, dereva mmoja, ulinzi na usalama wa lazima kwa ajili yake na mkewe, gharama za mazishi kwa ajili yake na mke wake na matumizi ya sehemu ya mapumziko ya wageni mashuhuri (VIP lounge).

Alieleza kuwa lengo la marekebisho hayo ni kudumisha hadhi ya Makatibu Wakuu Viongozi wastaafu na kutambua mchango wao wakati wa utumishi wao kwa serikali.

Kuhusu CAG, mwanasheria huyo alisema kimeongezwa kifungu kipya cha 4A baada ya kifungu cha 4 kinachohusu stahili na marupurupu ya CAG.

Alibainisha kuwa licha ya masharti ya sheria nyingine yoyote iliyoandikwa, Rais atakuwa na mamlaka ya kuamua au kurekebisha mshahara, marupurupu na manufaa mengine ya CAG wakati akiwa kazini, anapostaafu, anapoondolewa kazini au anapojiuzulu.

Alisema katika kutekeleza mamlaka chini ya kifungu kidogo cha (1), Rais atazingatia masharti ya Ibara ya 144(6) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na asili ya majukumu ya CAG na kwamba

marekebisho hayo yamezingatia zuio la CAG kutokushika nafasi yoyote ya madaraka baada ya kustaafu utumishi.

Akichangia mjadala wa miswada hiyo, Mbunge wa Madaba (CCM), Dk. Joseph Mhagama, alisema namna ambavyo Makatibu Wakuu Viongozi wanapotoa muda wao kuwatumikia watanzania kupitia sekta ya utumishi wa umma, hawapati fursa ya kufanya shughuli nyingine.

"Huyu ni mmoja kati ya viongozi muhimu sana katika taifa letu. Sisi kamati tulijiridhisha tuna mihimili hiyo mitatu na ndani ya mhimili wa serikali kuna baadhi ya maeneo ambayo watumishi wake wanahitaji motisha ya hali ya juu ili wafanye kazi kwa uadilifu na uzalendo mkubwa.

"Tumetoa tahadhari kuwa Katibu Mkuu Kiongozi baada ya kumaliza kazi ya ukatibu mkuu kiongozi huwa anateuliwa kwa jukumu lingine, kuna wengine tumeona walipata nafasi za ubalozi na kupelekwa vituo vya kazi, katika mazingira kama haya tumeona serikali ifikirie kuhusu utaratibu huu," alisema.

Alieleza kuwa kwa kuwa kiongozi huyo anapostaafu anakuwa amewekewa utaratibu mzuri wa kustaafu, ni vizuri baada ya kumaliza majukumu ya nafasi hiyo astaafu ili nafasi zingine wapewe watanzania wenye sifa zinazotosha.

Mbunge wa Nkenge (CCM), Florent Kyombo, alisema utumishi wa viongozi hao serikalini unahitaji weledi na umakini, uzalendo na kujitoa katika kusimamia majukumu kwenye maeneo waliyopangiwa.

"Kwa mfano CAG, majukumu yake yanahitaji weledi na uzalendo mkubwa. Sasa baada ya kustaafu kunaonekana kuna wasiwasi mbele, inaweza kuingilia msimamo wake wa kufanya kazi kwa weledi na uzalendo.

"Anapoona serikali imemjali, imemwekea utaratibu mzuri baada ya kazi yake kwa kuwa kazi anayoifanya wakati mwingine kuna msigano ndani yake, wakati mwingine anapostaafu anaweza kukosa huduma mbalimbali hata kwa watu wanaomzunguka," alisema.

Awali, akisoma maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria, Florent Kyombo alishauri serikali kufanya rejea sahihi ya Ibara ya 142(3) na Ibara ya 144(6) ambazo zinaweka masharti ya mtumishi wa serikali anayehusika na masharti ya Ibara ya 142(3), maslahi yake hayatabadilishwa kwa maana ya kupunguzwa na hatateuliwa kushika au kushikilia madaraka ya kazi nyingine yoyote katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mtawalia.

***Kwa maoni; +255 677 020 701***
***Email; costumerrelations@guardian.co.tz***

## Samia kuzindua Sera ya Elimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan kesho anatarajiwa kuzindua Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 jijini Dodoma yenye lengo la kuleta mageuzi ya utoaji elimu nchini.

Miongoni mwa mageuzi yaliyomo katika sera hiyo ni kufundishwa kwa somo la TEHAMA, mafunzo ya ufundi stadi kuanzia elimu ya msingi na matumizi ya akili unde (AI).

Akizungumza jana jijini hapa, Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa alisema lengo la kufanyiwa mapitio hayo ya sera ni kuwafanya wanafunzi kuwa na umahiri na ujuzi unaoakisi mahitaji kitaifa na kimataifa ili kushindana na kushiriki kikamilifu kwenye soko la ajira duniani.

Alisema sera hiyo itazalisha wanafunzi wenye maarifa, maadili na ujuzi utakaowawezesha wahitimu kwenye ngazi mbalimbali kujiajiri na kuajiri wengine na kuongeza uwezo wa ushindani kwenye soko hilo.



Msigwa ambaye ni Katibu Mkuu Wizara, Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, alisema mapitio hayo yameshirikisha wadau na matokeo makubwa yanatarajiwa kwa kuwa huduma ya elimu inagusa jamii moja kwa moja.

Alisema Rais hakupendezwa na wanafunzi kuhitimu shahada huku wakiwa hawana ujuzi katika uzalishaji.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo alisema sera hiyo itazinduliwa sambamba na vitendea kazi ikiwamo mkakati wa utekelezaji sera ambao tayari umeandaliwa.

Alisema sera hiyo ilielekeza kuboresha mitaala ya elimu ambayo imeboreshwa kwa ngazi zote kuanzia ngazi ya awali na vyuo vikuu kwa sasa vinaendelea kuboresha.

Alisema mitaala hiyo ni pamoja na wa elimu ya awali, elimu ya msingi kuanzia darasa la kwanza hadi la sita, elimu ya sekondari ngazi ya chini na juu na mafunzo ya ualimu ambayo ilianza kutumika mwaka jana na matunda yameanza kuonekana.

Katibu Mkuu alisema kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, sekta ya elimu kupitia sera hiyo umeandaliwa mkakati wa matumizi ya TEHAMA katika kujenga uchumi wa kidigitali.


### JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA MTWARA, LINDI NA RUVUMA KATIKA HALMASHAURI ZA WILAYA ZA MADABA, NAMTUMBO NA TUNDURU.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma katika Halmashauri za Wilaya za Madaba, Namtumbo na Tunduru tarehe 28 Januari hadi 03 Februari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumanne tarehe 28 Januari hadi siku Jumatatu tarehe 03 Februari, 2025
2. **VITUO:** Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi ambao hawakuwahi kuandikishwa hapo awali, na ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka
2. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi (Jimbo au Shehia).
3. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
4. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
5. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili kwa pamoja, wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume ***www.inec.go.tz*** au anuani ya ***ovrs.inec.go.tz*** kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la shehia anayokusudia kuhamia, kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo katika kituo cha kuandikisha Wapiga Kura ili kukamilisha taratibu na kupatiwa kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) anaweza kuingia kwenye mfumo wa OVRS kwa kupiga *152*00#, kisha, atachagua namba 8 na kubonyeza, kisha atachagua namba 2, kisha atabonyeza namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga simu namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali na hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

***KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***

**Limetolewa leo tarehe 20 Januari, 2024 na:**

**Christina P. Ballali**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

# Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

Amana Bank
*Pamoja, katika njia sahihi*

**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2024**

| | SHS '000<br>Robo Mwaka/ Mwaka wa sasa<br>31 - 12 - 2024 | SHS '000<br>Robo Mwaka iliopita<br>30 - 09 - 2024 |
|---|---|---|
| **A. MALI** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 13,096,646 | 14,396,319 |
| 2. Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 40,354,921 | 27,882,284 |
| 3. Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 0 | 0 |
| 4. Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 11,497,078 | 13,957,394 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 206,796 | 278,274 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 24,451,874 | 31,936,228 |
| 10. Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 1,000,719 | 1,000,479 |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 197,014,479 | 194,034,607 |
| 12. Mali Nyingine | 9,595,999 | 10,522,888 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| 14. Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 10,367,823 | 9,913,607 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **307,586,336** | **303,922,080** |
| | 0 | 0 |
| **B. DHIMA** | 0 | 0 |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 18,206,000 | 0 |
| 18. Amana za Wateja | 219,863,153 | 231,504,226 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20. Amana Maalumu | 15,768,031 | 20,961,851 |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 113,349 | 119,399 |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 4,186,182 | 2,185,035 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 18,614 | 135,126 |
| 27. Dhima Nyingine | 10,703,840 | 11,440,201 |
| 28. Madeni | 6,750,000 | 6,750,000 |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | 275,609,168 | 273,095,838 |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **31,977,168** | **30,826,242** |
| | | |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 45,060,215 | 45,060,215 |
| 32. Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (19,468,816) | (19,468,816) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 6,385,769 | 5,234,843 |
| 35. Akaunti Nyingine za Mtaji | 0 | 0 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **31,977,168** | **30,826,242** |
| | | - |
| 38.Dhima Zisizo Dhahiri | 17,198,843 | 17,198,843 |
| 39. Mikopo Chechefu | 11,392,611 | 11,392,611 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 9,145,595 | 9,145,595 |
| 41. Mali Nyingine Chechefu | 275,046 | 275,046 |
| | | |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 10.4% | 10.1% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.1% | 5.2% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 81.2% | 80.5% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 67.0% | 66.9% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 75.3% | 77.7% |
| (vi) Ongezeko la Amana | 0.5% | 1.1% |
| (vii) Ongezeko la Mali | 1.2% | 1.9% |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA 2024**

| | SHS'000<br>Robo ya Mwaka sasa | SHS'000<br>Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | SHS'000<br>Limbikizo la Mwaka wa sasa | SHS'000<br>Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|
| | **31 - 12 - 2024** | **31 - 12 - 2023** | **31 - 12 - 2024** | **31 - 12 - 2023** |
| 1. Faida itokanayo na Mikopo | 7,762,426 | 6,392,353 | 28,879,091 | 22,229,204 |
| 2. Gawio la Faida kwa waweka Amana | (894,150) | (427,552) | (1,946,228) | (1,873,278) |
| 3. Mapato Halisi ya Faida (1kutoa 2) | 6,868,277 | 5,964,801 | 26,932,863 | 20,355,926 |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | (418,615) | (121,063) | -2,986,307 |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | -217,981 | (1,087,161) | -2,953,194 | (2,793,732) |
| | | | | |
| **6. Faida isiyotokana na Mikopo:** | **2,447,855** | **2,224,133** | **9,098,962** | **7,767,576** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 370,959 | 353,895 | 1,722,875 | 1,121,702 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 2,076,896 | 1,870,238 | 7,376,087 | 6,645,874 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **7. Gharama za uendeshaji:** | **(6,679,602)** | **(5,747,155)** | **(23,498,930)** | **(21,523,153)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (3,372,246) | (2,324,546) | (11,422,283) | (9,476,791) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7.3 Gharama Nyingine | (3,307,355) | (3,422,609) | (12,076,648) | (12,046,362) |
| 8. Faida /(Hasara) ya Uendeshaji | 2,418,550 | 936,003 | 9,458,638 | 820,310 |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | (1,267,624) | 453,970 | (3,072,869) | (424,670) |
| **10. Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | 1,150,927 | 1,389,973 | 6,385,769 | 395,640 |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **1,150,927** | **1,389,973** | **6,385,769** | **395,640** |
| | | | | |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 349 | 328 | 349 | 328 |
| 14. Mapato kwa Hisa | 2.6% | 3.1% | 14.2% | 0.9% |
| 15. Idadi ya Matawi | 10 | 10 | 10 | 10 |
| | | | | |
| BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.38% | 0.51% | 2.10% | 0.30% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 4% | 1% | 20% | 2% |
| (iii) Uwiano wa Gharama za uendeshaji na Mapato Ghafi | 65% | 67% | 65% | 74% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya yatokanayo na Mikopo na Wastani wa Mali | 3% | 67% | 12% | 12% |
| | | | | |

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2024**

| | SHS'000<br>Robo Mwaka Mwaka wa sasa<br>31 - 12 - 2024 | SHS'000<br>Robo Mwaka Uliopita<br>30 - 09 - 2024 |
|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 1,150,927 | 2,065,128 |
| Marekebisho kwa Ajili ya | - | - |
| - Uchakavu Katika Mali | 745,685 | 1,313,792 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| - Gharama za ukodishaji | 136,771 | 136,771 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,979,872) | (5,909,610) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 1,371,107 | 2,680,354 |
| - Mabadiliko ya kiwango kinachohitajika na banki kuu kisheria | (118,113) | (144,867) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (1,142,223) | (832,328) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 2,850,557 | (3,599,975) |
| - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| - Kodi Iliyolipwa | (140,000) | (140,000) |
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | **1,874,838** | **(4,430,735)** |
| | - | - |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaj** | - | - |
| Gawio Lililopokewa | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (184,260) | (226,325) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | (40,322) | (36,816) |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Marekebisho katika mali za Kudumu | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(224,582)** | **(263,142)** |
| | - | - |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha** | - | - |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (394,967) | (394,967) |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | (394,967) | (394,967) |
| | - | - |
| | - | - |
| **Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **1,255,289** | **(5,088,844)** |
| | - | - |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu kwa robo mwaka iliyopita | 74,147,819 | 79,236,663 |
| | - | - |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa robo Mwaka** | **75,403,107** | **74,147,819** |
| | | |

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2024**

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyo-bakizwa | Ziada ya Kisheria | Mengi-neyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa sasa 2024 | | | | | | |
| | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 45,060,215 | 0 | (19,468,815) | - | 0 | 25,591,400 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 6,385,769 | 0 | 0 | 6,385,769 |
| Share zilizouzwa | - | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | - | - | 0 | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **45,060,215** | 0 | **(13,083,047)** | 0 | 0 | **31,977,168** |
| | 0 | | 0 | 0 | | 0 |
| Mwaka Uliopita 2023 | 0 | | 0 | 0 | | 0 |
| | 0 | | 0 | 0 | | 0 |
| Salio la mwanzo wa Mwaka | 45,060,215 | 0 | (21,067,846) | 1,203,391 | 0 | 25,195,760 |
| salio la mwanzo la bamadilio ya utaraibu wa kihasibu nanber 9 | 0 | 0 | 395,640 | 0 | 0 | 395,640 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 1,203,391 | (1,203,391) | 0 | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **45,060,215** | 0 | **(19,468,815)** | - | 0 | **25,591,400** |

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

Jina na cheo

**Abubakar Athman**
(Mkurugenzi Mtendaji) — Imesainiwa Januari 29, 2025

**CPA Saidi Mbaruku**
(Mkuu wa fedha) — Imesainiwa Januari 29, 2025


**CPA Mwinyi Sekro**
(Mkuu wa Ukaguzi) — Imesainiwa Januari 29, 2025

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

**Joseph Gonsalves**
(Mwenyekiti) — Imesainiwa Januari 29, 2025

**Salem Balleith**
(Mkurugenzi) — Imesainiwa Januari 29, 2025

BADO UNAHANGAIKA KULIPIA MWANAO ADA YA SHULE?
Piga 0657 980 000 Sasa, ujue kuhusu
Amana Bank
Together, on the right path
Elimu Financing
0657 980 000 /amanabanktz /amanabank



183508

**TANGAZO**

# Tariff Guide 2024

*Effective: 01/06/2024*

Amana Bank
*Together, on the right path*

| | PRODUCT/SERVICES | LOCAL CURRENCY (TZS) | FOREIGN CURRENCY(USD, EUR, GBP, AED) |
|---|---|---|---|
| 1 | **SAVINGS ACCOUNTS (Personal/Joint/Annisaa Account) - (Under Wadia Contract)** | | |
| | Minimum opening balance | 20,000 | USD, EUR, GBP 50, AED 150 |
| | Account maintenance balance | 10,000 | USD ,EUR ,GBP 50, AED 150 |
| | Limit on withdrawal | No limit | No limit |
| | Monthly maintenance fee | 2,000 | Free |
| | Over the counter withdrawal fee | Below TZS 1,000,000- TZS 4,500, 1,000,001- 10,000,000- 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 | Below USD, EUR, GBP 1,000 - 0% |
| | Limit on withdrawal | No limit | N/A |
| | Over the counter withdrawal (above TZS 10,000,000) | 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | Over USD, EUR, GBP 1,000 - 0.25% |
| | Over the counter balance enquiry fee | 500 | N/A |
| | Bank statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP Equivalent |
| | Bank statements above twelve months | 20,000 per statement | USD, EUR, GBP Equivalent |
| | Electronic statement | Free | Free |
| 2 | **STUDENT ACCOUNT (Under Wadia Contract)** | | |
| | Minimum opening balance | 10,000 | N/A |
| | Account maintenance balance | 10,000 | N/A |
| | Limit on withdrawal | No limit | N/A |
| | Monthly maintenance fee | Free | N/A |
| | Over the counter withdrawal fee | Below TZS 1,000,000- TZS 4,500, 1,000,001- 10,000,000- 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 | N/A |
| | Limit on withdrawal | No limit | N/A |
| | Over the counter withdrawal ( above TZS 10,000,000 ) | Above 10,000,000 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Over the counter balance enquiry fee | 500 | USD, EUR, GBP Equivalent |
| | Bank statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP Equivalent |
| | Bank statements above twelve months | 20,000 per statement | N/A |
| | Electronic statement | Free | N/A |
| 3 | **KILIMANJARO DIASPORA ACCOUNT (Under Wadia Contract)** | | |
| | Minimum opening balance | 50,000 | USD, EUR, GBP 50, AED 250 |
| | Account maintenance balance | 50,000 | USD, EUR, GBP 50, AED 150 |
| | Limit on withdrawal | No limit | No limit |
| | Monthly maintenance fee | Free | Free |
| | Over the counter withdrawal fee | Below TZS 1,000,000 - TZS 4,500, From 1,000,001 to 10,000,000 - 0.18% of the amount Minimum TZS 18,000 and Maximum TZS 180,000 | 1.2% minimum USD, EUR, GBP 6 |
| | Limit on withdrawal | No limit | N/A |
| | Over the counter withdrawal (above TZS 10,000,000 ) | Above 10,000,000 - 0.18% of the whole amount, Minimum fee TZS 18,000 Maximum fee TZS 180,000 Fees may be waved if a prior notice of at least 5 days is given | N/A |
| | Over the counter balance enquiry fee | 500 | USD, EUR, GBP 1 |
| | Bank statements (monthly, quarterly, annually) | Free | USD, EUR, GBP 1 USD, EUR, GBP 4 Per Statement |
| | Second and subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 10 Per Statement |
| | Bank statements above twelve months | 20,000 per statement | Free |
| | Electronic statement | Free | Free |
| 4 | **ASHRAF ACCOUNT (Under Wadia Contract)** | | |
| | Minimum opening balance | 1,000,000 | USD, EUR, GBP, AED 500 |
| | Account maintenance balance | 100,000 | USD, EUR, GBP/GBP/EURO/ AED 100 |
| | Monthly maintenance fee | 20,000 | USD, EUR, GBP/GBP/EURO 10, AED 35 |
| | Over the counter withdrawal fee | Below TZS 1,000,000 - TZS 4,500, 1,000,001 - 10,000,000- 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 | Below USD, EUR, GBP 1,000 - 0% Over USD, EUR, GBP 1,000 - 0.25% |
| | Limit on withdrawal | No limit | N/A |
| | Over the counter withdrawal (above TZS 10,000,000) | 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Bank statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 4.0 Per Statement |
| | Electronic statement | Free | Free |
| 5 | **BODABODA ACCOUNT - (Under Wadia Contract)** | | |
| | Minimum opening balance | 10,000 | N/A |
| | Account maintenance balance | 10,000 | N/A |
| | Limit on withdrawal | No limit | N/A |
| | Monthly maintenance fee | Free | N/A |
| | Over the counter withdrawal fee | Below TZS 1,000,000- TZS 4,500, 1,000,001- 10,000,000- 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 | N/A |
| | Over the counter withdrawal (above TZS 10,000,000 ) | Above 10,000,000 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Over the counter balance enquiry fee | 500 | N/A |
| | Bank statements (monthly) | Free | N/A |
| | Second and subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | N/A |
| | Bank statements above twelve months | 20,000 per statement | N/A |
| | Electronic statement | Free | N/A |
| 6 | **NAFUU ACCOUNT - (Under Wadia Contract)** | | |
| | Minimum opening balance | 10,000 | N/A |
| | Account maintenance balance | 10,000 | N/A |
| | Monthly maintenance fee | Free for all accounts maintaining a monthly turn-over TZS 2,500,000. All account turn-over balance above TZS 2,500,000 will be charged TZS 1,500 monthly | N/A |
| | Limit on withdrawal | No limit | N/A |
| | Over the counter withdrawal fee | Below TZS 1,000,000 - TZS 4,500, 1,000,001- 10,000,000- 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 | N/A |
| | Over the counter withdrawal limit (above TZS 10,000,000) | Above 10,000,000 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Over the counter balance enquiry fee | Free | N/A |
| | Bank statements (monthly) | Free | N/A |
| | Second and subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | N/A |
| | Bank statements above twelve months | 20,000 per statement | N/A |
| | Electronic statement | Free | N/A |
| 7 | **HAJJ & UMRAH SAVINGS ACCOUNT** | | |
| | Minimum opening balance | 10,000 | USD, EUR, GBP 50, AED 150 |
| | Account maintenance balance | 10,000 | USD, EUR, GBP 50, AED 150 |
| | Profit participation balance (Min. daily balance) | 100,000 | USD, EUR, GBP 1,000, AED 150 |
| | Limit on withdrawal | Twice Annually | Twice Annually |
| | Monthly maintenance fee | Free | Free |
| | Over the counter withdrawal fee | Free - Twice annually | Free - Twice annually |
| | Bank statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 4 Per Statement |
| | Electronic statement | Free | Free |
| | Hajj Time SMS Alert | Free | Free |
| 8 | **NURU SAVINGS ACCOUNT (Children Account)** | | |
| | Minimum opening balance | 10,000 | USD, EUR, GBP 50, AED 150 |
| | Account maintenance balance | 10,000 | USD, EUR, GBP 50, AED 150 |
| | Profit participation balance (Min. daily balance) | Above 100,000 | USD, EUR, GBP 1,000, AED 150 |
| | Limit on withdrawal | Four times in a year | Four times in a year |
| | Charge on withdrawal exceeding 4 allowable withdraws per year | 12,000 | USD, EUR, GBP 6 |
| | Monthly maintenance fee | Free | Free |
| | Bank statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 4 Per Statement |
| | Electronic statement | Free | Free |
| 9 | **SALARY SAVINGS ACCOUNT - (Under Wadia Contract)** | | |
| | Minimum opening balance | 0 | 0 |
| | Account maintenance balance | 2,000 | USD, EUR, GBP 5 |
| | Monthly maintenance fee | 1,000 | Free |
| | Over the counter withdrawal (above TZS 10,000,000) | 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | Over USD, EUR, GBP 1,000 - 0.25% |
| | Over the counter withdrawal fee | Below TZS 1,000,000 - TZS 4,500, 1,000,001- 10,000,000- 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 | USD, EUR, GBP 2 |
| | Bank statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 4 Per Statement |
| | Electronic statement | Free | N/A |
| 10 | **MAFAO SAVINGS ACCOUNT - (Under Mudharabah Contract)** | | |
| | Minimum opening balance | 10,000 | NA |
| | Account maintenance balance | Free | NA |
| | Monthly maintenance fee | Free | NA |
| | Over the counter withdrawal fee | Below TZS 1,000,000- TZS 4,500, 1,000,001- 10,000,000- 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 | NA |
| 11 | **PERSONAL CURRENT ACCOUNT** | | |
| | Minimum opening balance | 50,000 | USD, EUR, GBP 50, AED 150 |
| | Account maintenance balance | 50,000 | USD, EUR, GBP 50, AED 75 |
| | Monthly maintenance fee | 11,000 | USD, EUR, GBP 11, AED 50 |
| | Over the counter withdrawal fee | Below TZS 500,000-3000, 500,001-1,000,000 - 3,500, 1,000,001-5,000,000- 4,500, 5,000,00-25,000,000-6,500, Above 25,000,000-15,000 | USD, EUR, GBP 0.5% |
| | Bank statements (monthly) | Free | Free |
| | Electronic statement | Free | Free |
| | Second and subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 4 Per Statement |
| | Electronic statement | Free | Free |
| | Profit participation balance (Min. daily balance) | N/A | USD, EUR, GBP, AED 200 |
| 12 | **CORPORATE CURRENT ACCOUNT** | | |
| | Minimum opening balance | 100,000 | USD, EUR, GBP500, AED300 |
| | Account maintenance balance | 100,000 | USD, EUR, GBP100, AED300 |
| | Monthly maintenance fee | 20,000 | USD, EUR, GBP, AED 20 |
| | Over the counter withdrawal fee | Below TZS 5,000,000-5,000, 5,000,001-20,000,000-7,000, 20,000,001-50,000,000-9,000, 50,000,001-100,000,000- 15,000, Above 100,000,000-30,000 | USD, EUR, GBP 0.5% |
| | Activation of dormant account | Free | Free |
| | Certificate of balance to auditors/ reference letters | 10,000 | USD, EUR, GBP 5 |
| | Bank statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 4 Per Statement |
| | Electronic statement | Free | Free |
| 13 | **BIASHARA CURRENT ACCOUNT (SMEs)** | | |
| | Minimum opening balance | 50,000 | USD, EUR, GBP 50, AED 150 |
| | Account maintenance balance | 50,000 | USD, EUR, GBP 50, AED 75 |
| | Monthly maintenance fee | 15,000 | USD, EUR, GBP, AED 15 |
| | Over the counter withdrawal fee | Below TZS 500,000 -3000, 500,001- 1,000,000 - 3,500, 1,000,001 - 5,000,000 - 4,500, 5,000,001- 25,000,000 - 6,500, Above 25, 000,000 - 15,000 | USD, EUR, GBP 0.5% |
| | Certificate of balance to auditors/ reference letters | 10,000 | USD, EUR, GBP 5 |
| | Activation of dormant account | Free | Free |
| | Bank statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and subsequent bank statement copy (ies) | 6,000 Per Statement | USD, EUR, GBP 4 Per Statement |
| | Electronic statement | Free | Free |
| | Profit participation balance (Min. daily balance) | N/A | USD, EUR, GBP, AED 250 |
| 14 | **NGO CURRENT ACCOUNT** | | |
| | Minimum opening balance | 100,000 | USD, EUR, GBP100, AED150 |
| | Account maintenance balance | 0 | USD, EUR, GBP100, AED150 |
| | Monthly maintenance fee | 0 | 0 |
| | Over the counter withdrawal fee | 3,000 | Below USD, EUR, GBP 1,000 - 0% Over USD, EUR, GBP 1,000 - 0.25% |
| | Certificate of balance to auditors/ reference letters | 10,000 | USD, EUR, GBP 5 |
| | Activation of dormant account | Free | Free |
| | Bank statements (monthly) | Free | Free |
| | Second and subsequent bank statement copy(ies) | 2,000 Per Page | USD, EUR, GBP 1 Per Page |
| | Electronic statement | Free | Free |
| 15 | **IHSAAN CURRENT ACCOUNT** | | |
| | Minimum opening balance | 0 | 0 |
| | Account maintenance balance | 0 | 0 |
| | Over the counter withdrawal fee | 0 | 0 |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | **639%** | **561%** |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Hali na Mali | **76%** | **70%** |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | **85%** | **81%** |
| (vi) | Ongezeko la Amana | **-4.5%** | **0.0%** |
| (vii) | Ongezeko la Mali | **-0.6%** | **9.9%** |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31/122024 | Robo ya Mwaka Linganishi 31/12/2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/12/2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31/12/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS | TZS | TZS |
| 1 | Mapato ya Riba | 5,896 | 4,894 | 22,135 | 17,116 |
| 2 | Gharama za Riba | 1,231 | 904 | 4,505 | 1,957 |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2 )** | **4,665** | **3,990** | **17,631** | **15,159** |
| | | - | - | - | - |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (466) | **(596)** | (1,191) | **(1,156)** |
| | | - | - | - | - |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,274** | **1,400** | **6,065** | **4,638** |
| | | - | - | - | - |
| | 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (121) | 201 | 174 | 477 |
| | 6.2 Ada za Kamisheni | 864 | 903 | 4,065 | 3,064 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 532 | 296 | 1,826 | 1,097 |
| | | - | - | - | - |
| 7 | **Gharama Zisizo na Riba :** | **4,998** | **5,220** | **20,350** | **17,886** |
| | | - | - | - | - |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 2,819 | 2,359 | 10,312 | 8,674 |
| | 7.2 Gharama Nyingine | 2,179 | 2,861 | 10,039 | 9,212 |
| | 7.3 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | | - | - | - | - |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **475** | **(426)** | **2,154** | **755** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 147 | - | 489 | - |
| 10 | **Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **328** | **(426)** | **1,665** | **755** |
| | | 0 | - | - | - |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | **486** | **441** | **486** | **441** |
| 12 | Mapato kwa Hisa | 14,442 | (20,078) | 73,272 | 35,606 |
| 13 | Kipato kwa Hisa | 14,442 | (20,078) | 73,272 | 35,606 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| 15 | Vituo Vya Biashara | 35 | 35 | 35 | 35 |
| 16 | Vituo Vidogo | 12 | 12 | 12 | 12 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | - | - | - |
| (i) | Uwiano wa Mapato na Wastani wa Mali | 0.5% | -0.8% | 2.5% | 1.4% |
| (ii) | Uwiano wa Mapato na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.2% | -1.8% | 6.1% | 3.1% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 84% | 97% | 86% | 90% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani Wa Mali Zinazozalisha | **17%** | **18%** | **63%** | **68%** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA

Katika kuaandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Chilala Hakooma(Ofisa Mtendaji Mkuu) | | 15 Januari 2025 |
| Rogathe Godson (Mkuu wa Fedha) | | 15 Januari 2025 |
| Albert Chikira (Mkaguzi mkuu wa Ndani) | | 15 Januari 2025 |

Sisi,tuliotajwa hapo chini,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifaza zahapo juu,Tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| | Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| 1 | Athanasia Soka ( Mwenyekiti ya Bodi) | | 15 Januari 2025 |
| 2 | Jeff Mckrae (Mwendeshaji) | | 15 Januari 2025 |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa Tarehe 31/12/2024 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 30/09/2024 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31/12/2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 31/12/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS | TZS | TZS |
| I: | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULI ZA UENDESHAJI** | | | | |
| | Mapato/(Hasara)Hakisi | **328** | **474** | **1,665** | **755** |
| | | - | - | - | - |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - | - | - |
| | Hasara Katika Mali | 159 | 152 | 597 | 541 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (3,566) | (415) | (8,630) | (12,958) |
| | Faida/Hasira Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | (384) | (4) | 448 | 601 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (251) | (965) | (1,227) | (995) |
| | Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| | Mengineyo | (1,173) | 1,846 | 630 | (589) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | - | - | - | - |
| | **kwa shughuli za uendeshaji** | **(4,887)** | **1,089** | **(6,517)** | **(12,646)** |
| | | - | - | - | - |
| II: | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTIKANA NA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI** | - | - | - | - |
| | Gawio Lililopokelewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (334) | (215) | (1,343) | (1,010) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | - | - | - | - |
| | **kwa Shughuli za uekezaji** | **(334)** | (215) | (1,343) | (1,010) |
| | | - | - | - | - |
| III: | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULIZA KIFEDHA** | - | - | - | - |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | **(768)** | 4,012 | 3,227 | 17,907 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 1,811 | 59 | 3,070 | 1,146 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo | (209) | (332) | (954) | 1,655 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | - | - | - | - |
| | **kwa Shughuli za Kifedha** | **834** | **3,739** | **5,343** | **20,709** |
| | | - | - | - | - |
| IV: | **FEDHA TASLIMU NA MALI ZAINAZOFANANA NA FEDHA TASLIMU** | - | - | - | - |
| | Onzezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofana na Fedha Tastimu | (4,387) | 4,614 | (2,517) | 7,053 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 14,491 | 9,878 | 12,622 | 5,569 |
| | | - | - | - | - |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu /** | - | - | - | - |
| | **Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **10,105** | **14,491** | **10,105** | **12,622** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2024
(Kiasi cha shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa Mwaka (2024)** | **21,200** | **(1,646)** | **0** | **5,076** | **24,630** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | **1,665** | - | - | **1,665** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | **4,607** | **(473)** | - | **(2,019)** | **2,116** |
| **Salio la mwisho wa Robo ya mwaka wa sasa** | **25,807** | **(454)** | **0** | **3,057** | **28,411** |
| | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwanzo wa Mwaka Uliopita ( 2023)** | **21,200** | **(2,418)** | **0** | **2,292** | **21,074** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | **755** | - | - | **755** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | **17** | - | **2,784** | **2,801** |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **21,200** | **(1,646)** | **0** | **5,076** | **24,630** |

## ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA

ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA

| **Huduma za Kibenki** | | | | | **Gharama-(Pamoja na VAT)** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kuangalia Salio-Dirishani & ATM | | | | 554 |
| 2 | Kuhamisha fedha | Ndani ya VFT hadi TZS1,000,000 | | | 944 |
| | | Ndani ya VFT zaidi ya TZS1,000,000 | | | 1,180 |
| | | Kwenda Benki nyingine hadi TZS10,000,000 | | | 3,554 |
| | | Kwenda Benki Nyingine zaidi ya TZS10,000,000 | | | 11,800 |
| 3 | Kutoa disrishani hadi/Kwakila TZS 5,000,000 | | | | 1,770 |
| 4 | Kutoa ATM | | | | 1,500 |
| 5 | Kadi ya ATM (Mpya au Kubadili) | | | | 5,000 |
| 6 | Gharama za mwezi (Monthly Acc maintanance fees) | Akiba Akaunti | | | 885 |
| | | Akaunti ya Biashara | | | 1,770 |
| 7 | Kufunga Akaunti | Akaunti ya Akiba, Watoto & Dunduliza | | | 2,360 |
| | | Akaunti ya Vikundi na Biashara | | | 5,900 |
| 8 | Taarifa ya Akaunti | Taarifa Fupi ATM | | | 720 |
| | | Miezi 0-1 | | | Bure |
| | | Miezi 1-3 | | | 1,180 |
| | | Miezi 3-12 | | | 3,540 |
| | | Miezi 12-24 | | | 11,800 |
| | | Miezi 24-48 | | | 29,500 |
| | | Miaka 3-6 | | | 41,300 |
| | | Zaidi ya miaka 6 | | | 55,400 |
| **Huduma Za Simu (Mobile banking)** | | | | | **Gharama-(Pamoja na VAT)** |
| 9 | Kujua Salio-Simu | | | | 118 |
| 10 | Kutoa kwa simu-Kuanzia tarehe 1 Decemba 2024 | Kiwango cha chini | Kiwango cha juu | | |
| | | Chini ya 100,000 | | | 1,180 |
| | | 100,000 | 199,999 | | 1,770 |
| | | 200,000 | 299,999 | | 2,360 |
| | | 300,000 | 399,999 | | 2,950 |
| | | 400,000 | 499,999 | | 3,540 |
| | | 500,000 | 1,000,000 | | 4,720 |
| 11 | Kuhamisha Fedha-Simu | | | | 118 |
| 12 | Taarifa Fupi-Simu | | | | 354 |
| 13 | Kubadili Number ya Siri | | | | 236 |

**Akaunti**

| s/n | Huduma | Kiwango cha chini | Riba Kwa mwaka * |
|---|---|---|---|
| 1 | Akiba Akaunti | 5,000 | 3% |
| 2 | Salary Akaunti | 5,000 | 3% |
| 3 | Kikundi Akaunti | 20,000 | 4% |
| 4 | Watoto Akaunti | 10,000 | 4% |
| 5 | Biashara Akaunti | 100,000 | 3% |
| 6 | Fixed Deposit Accounts | N/A | Kulingana na muda na Kiasi |
| 7 | Dunduliza Akaunti | 10,000 | 4% |

** Riba kwa akaunti za aina zote itajilimbikiza kwa kila la siku kwa kiasi cha akiba cha TZS100,000 na kuendelea na kulipwa kila Mwezi.*

**Mikopo ya Vikundi**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo | Ada ya usimamizi wa Majanga |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mikopo ya Vikundi -Biashara group Loan | 5% | 60% | 3% | 1% |
| 2 | Mikopo ya Vikundi/Savings Group Loan | 5% | 60% | 2.5% | 0% |
| 3 | Mikopo ya Vikundi -Jiendeleze Group Loan | 4% | 48% | 3.1% | 1% |

**Mikopo Binafsi**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo | Ada ya usimamizi wa Majanga |
|---|---|---|---|---|---|
| 4 | Mkopo Binafsi Na shule- hadi TZS10M | 4% | 48% | 2.5% | 1% |
| 5 | Mkopo Binafsi na shule inayozidi TZS10M Hadi TZS 20M | 3.50% | 42% | 2.5% | 1% |
| 6 | Mikopo Binafsi na shuke inayozidi TZS20M | 2.50% | 30% | 2.5% | 1% |
| 7 | Elimisha | 4% | 48% | 3.5% | 1% |

**Mikopo ya Kilimo**

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo | Ada ya usimamizi wa Majanga |
|---|---|---|---|---|---|
| 9 | Mikopo Binafsi -Jikomboe Loan | 4% | 48% | 4.0% | 1% |
| 10 | Mikopo ya kikundi -Jitume | 5% | 60% | 4.0% | 1% |
| 11 | Mikopo ya Kikundi -Mkombozi Loan | 5% | 60% | 4.0% | 1% |
| 12 | Patnerships | 3% | 36% | 3% | 1% |

| | | |
|---|---|---|
| Chilala Hakooma(Ofisa Mtendaji Mkuu) | Sahihi | 15 Januari 2025 |
| Rogathe Godson (Mkuu wa Fedha) | Sahihi | 15 Januari 2025 |
| Albert Chikira (Mkaguzi mkuu wa Ndani) | Sahihi | 15 Januari 2025 |

## TANGAZO

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

UBA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZISIZOKAGULIWA KWA UMMA 31-12-2024

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya 31-Dec-24 | Robo Mwaka ya 30-Sep-24 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha taslimu | 3,981 | 3,367 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 8,256 | 11,003 |
| 3 | Uwekezaji katika amana za Serikali | 69,507 | 90,036 |
| 4 | Salio katika benki nyingine na taasisi za fedha | 22,458 | 4,332 |
| 5 | Hundi na miamala ya kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za wateja zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | - | 10,724 |
| 10 | Uwekezaji katika amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo halisi iliyopo | 34,232 | 51,946 |
| 12 | Mali nyingine | 7,970 | 15,528 |
| 13 | Uwekezaji wa hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali zisizohamishika, mitambo na vifaa | 4,067 | 3,960 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **150,471** | **190,896** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za benki nyingine na taasisi za fedha | - | - |
| 18 | Amana za wateja | 81,626 | 96,655 |
| 19 | Dhamana ya malipo kwa fedha taslimu | - | - |
| 20 | Amana maalumu | 4,997 | 6,513 |
| 21 | Maagizo ya malipo/fedha za kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na hawala za kibenki zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la kodi na gharama zitakazolipwa | 2,198 | 2,631 |
| 24 | Dhima la tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala isiyoshughulikiwa baina ya matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazolipwa baadae | 2,731 | 2,971 |
| 27 | Dhima nyingine | 3,828 | 3,505 |
| 28 | Madeni | 26,400 | 37,052 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **121,779** | **149,327** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **28,692** | **41,569** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa hisa uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | (29,759) | (37,993) |
| 34 | Faida (Hasara) ya kipindi husika | (4,576) | 8,308 |
| 35 | Akaunti nyingine za mtaji | 2,503 | 10,730 |
| 36 | Stahiki ya wenyehisa chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **28,692** | **41,569** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | 379,850 | 430,854 |
| 39 | Mikopo chechefu | 15,243 | 17,923 |
| 40 | Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 8,659 | 1,207 |
| 41 | Mali nyingine chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 19% | 22% |
| (ii) | Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 34% | 33% |
| (iii) | Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 50% | 52% |
| (iv) | Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 23% | 27% |
| (v) | Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 28% | 39% |
| (vi) | Ongezeko la amana | -16% | 0% |
| (vii) | Ongezeko la mali | -21% | 0% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 31-Dec-24 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Sep-24 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-24 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dec-23 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya riba | 4,422 | 4,890 | 22,349 | 20,852 |
| 2 | Gharama za riba | (5,601) | (1,209) | (8,814) | (5,440) |
| **3** | **Mapato halisi ya riba (1 kutoa 2)** | **(1,179)** | **3,680** | **13,535** | **15,412** |
| 4 | Madeni viza yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/ongezeko la tengo katika Mikopo | (8,263) | (447) | (9,073) | (1,428) |
| **6** | **Mapato yasiyo ya riba:** | **2,312** | **3,486** | **12,561** | **13,381** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | 794 | 1,729 | 6,559 | 6,371 |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 1,499 | 1,746 | 5,939 | 6,925 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato mengine | 19 | 11 | 63 | 85 |
| **7** | **Gharama zisizo za riba:** | **(5,255)** | **(4,657)** | **(19,645)** | **(18,143)** |
| | 7.1 Mishahara na mafao | (2,297) | (2,013) | (9,203) | (8,045) |
| | 7.2 Ada na kamisheni | (247) | (543) | (1,359) | (1,825) |
| | 7.3 Gharama nyingine | (2,711) | (2,101) | (9,083) | (8,272) |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya uendeshaji** | **(12,384)** | **2,063** | **(2,622)** | **9,222** |
| 9 | Tengo la kodi ya mapato | (500) | (488) | (1,954) | (735) |
| 10 | **Faida / (Hasara) halisi baada ya kodi ya mapato** | **(12,884)** | **1,575** | **(4,576)** | **8,487** |
| 11 | **Mapato mengine yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(12,884)** | **1,575** | **(4,576)** | **8,487** |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 128 | 143 | 128 | 143 |
| 14 | Mapato kwa hisa | (2,050) | 251 | (728) | 1,351 |
| **15** | **Idadi ya matawi** | 8 | 8 | 8 | 8 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i) Uwiano wa faida kabla ya kodi na wastani wa mali | -29.02% | 3.67% | -1.54% | 4.10% |
| | (ii) Uwiano wa faida baada ya kodi na wastani wa fedha za wanahisa | -146.70% | 18.88% | -13.03% | 25.44% |
| | (iii) Uwiano wa matumizi yasiyo ya riba na mapato ghafi | 78.03% | 55.59% | 56.27% | 53.00% |
| | (iv) Uwiano wa mapato halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | -3.37% | 7.49% | 9.67% | 7.84% |

| | ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|---|
| 1 | Gbenga Makinde<br>**Mkurugenzi Mtendaji** | ***Imesainiwa*** | *28 Januari2025* |
| 2 | Fina Andrew<br>**Kaimu Afisa Mkuu wa Fedha** | ***Imesainiwa*** | *28 Januari2025* |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | ***Imesainiwa*** | *28 Januari2025* |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| | ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|---|
| 1 | Amb.Tuvako Manongi<br>**Mkurugenzi** | ***Imesainiwa*** | *28 Januari2025* |
| 2 | Ebele Ogbue<br>**Mkurugenzi** | ***Imesainiwa*** | *28 Januari2025* |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka ya sasa 31-Dec-24 | Robo ya Mwaka linganishi 30-Sep-24 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-24 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dec-23 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **(12,884)** | **1,554** | **(4,576)** | **8,487** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | - | - | - |
| - Hasara Katika Mali | 8,746 | 1,074 | 9,820 | 1,418 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 2,243 | (3,304) | (1,062) | (6,814) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (16,545) | (13,207) | (29,751) | (18,840) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 20,529 | (44) | 20,485 | 11,832 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 8,214 | 665 | 8,879 | (712) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 7,558 | 11,571 | 19,129 | 16,058 |
| - Kodi Iliyolipwa | (500) | (1) | (501) | (570) |
| -Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **17,361** | **(1,692)** | **22,423** | **10,678** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (438) | (68) | (507) | (3,442) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(438)** | **(68)** | **(507)** | **(3,442)** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | (10,652) | 6,052 | 26,400 | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **(10,652)** | **6,052** | **26,400** | **-** |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **6,271** | **4,291** | **10,562** | **7,416** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | 23,181 | 18,890 | 18,890 | 20,081 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **29,452** | **23,181** | **29,452** | **27,497** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2024** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (37,795) | 10,730 | - | - | 33,459 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | (4,576) | - | - | - | (4,576) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | 8,227 | (8,227) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | (191) | - | - | - | (191) |
| Share issued | | | - | | - | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(34,335)** | **2,503** | **-** | **-** | **28,692** |
| **Mwaka uliopita 2023** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (39,925) | 5,097 | - | - | 25,696 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | 7,763 | - | - | - | 7,763 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | (5,633) | 5,633 | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | | | | | - | | |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,420** | **29,104** | **(37,795)** | **10,730** | **-** | **-** | **33,459** |

**United bank of Africa (T) Ltd** ni benki ya kiafrika inayoongoza Afrika kwa kutoa huduma za kibenki kwa wateja zaidi ya milioni 13 katika matawi zaidi ya 1000 barani Afrika, Marekani, Ulaya na Umoja wa Nchi za Kiarabu.

**Afrika Mashariki na Kusini** | **Afrika ya Kati** | **Afrika Magharibi** | **Ulaya** | **Marekani** | **Umoja wa Nchi za Kiarabu**

- Tanzania
- Kenya
- Congo DRC
- Mozambique
- Uganda
- Zambia

- Cameroon
- Gabon
- Tchad
- Congo Brazzaville

- Ghana
- Benin
- Burkina Faso
- Cote D'Ivore (CDI)
- Liberia
- Sierra Leone
- Senegal
- Mali
- Guinea

- UK
- France

- New York

- Dubai

30C/30D Barabara ya Nyerere, S.L.P 80514, Dar es Salaam, Tanzania. Simu: +255 789 784 302 | Barua Pepe: customerservicetz@ubagroup.com

ubatanzania



# Wakulima wa parachichi wajazwa 'manoti'

**Na Nebart Msokwa,** TUKUYU

WAKULIMA wa maparachichi wilayani Rungwe wamelipwa zaidi ya Sh. milioni 10 ambazo walikuwa wanaidai kampuni ya Mbembati Trading iliyokuwa ikinunua matunda hayo.

Kampuni hiyo imewalipa wakulima hao ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera ambaye aliipa saa 48 iwe imewalipa, huku akitishia kuichukulia hatua endapo isingetekeleza.

Akiwa kwenye ziara ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi wilayani Rungwe, Homera alipokea kero ya wakulima kudhurumiwa fedha zao na kampuni hiyo ambayo imekuwa ikinunua matunda kwa muda mrefu.

Baada ya kuibuliwa kero hiyo aliagiza wamiliki wa kampuni hiyo kuwalipa wakulima kabla serikali haijaanza kuwachukulia hatua za kisheria ikiwemo kuwakamata na kuwasweka 'selo'.

Juzi, kampuni hiyo iliwalipa wakulima fedha zote ambazo walikuwa wanadai huku ikieleza sababu za kuchelewesha malipo kuwa ni kutokana na kuharibika matunda yote ambayo iliyachukua kwa wakulima.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Erasto Mbembati alisema walisafirisha matunda hayo kwenda kuyaosha kwenye ghala lililopo Makambako mkoani Njombe kabla ya kuyasafirisha kwenda nchini India ambako ndiko kuna soko.

Alisema baada ya kuyafikisha Makambako na kuanza kuyaosha walibaini kuwa yalikuwa yameshambuliwa na fangasi na hivyo kusababisha kuwa na alama nyeusi.

Alisema baada ya kutokea tatizo hilo waliamua kuyatupa kutokana na kutokuwa na uwezekano wa kuyasafirisha kwenda sokoni akidai kuwa wangeharibu soko la zao hilo.

"Tulikuwa tumepata soko la tani 40 nchini India mwaka jana Machi, sasa tulipoyachukua na kuyasafirisha kwenda Njombe tulibaini mzigo umeharibika na hivyo tukautupa, kwa hiyo tumeingia hasara kubwa sana ndio maana tumechelewa kuwalipa wakulima hawa," alisema Mbembati.

Alisema kampuni yake imeingia hasara ya kuwalipa wakulima mzigo ambao uliharibika na pia ililazimika kulipa faini kutokana na kuwacheleweshea wanunuzi mzigo.

Hivyo, aliiomba Wizara ya Kilimo kuwasaidia wakulima dawa za kutibu matunda hayo ili yasiharibike na kuwasababishia hasara wanunuzi ambao wamekuwa wakinunua.

Baadhi ya wakulima waliolipwa fedha hizo waliishukuru serikali kwa kuwasaidia kupigania haki yao, huku wakiiomba kuweka mifumo mizuri ambayo itawasaidia kutoingia hasara.

Mmoja wa wakulima hao, Yusta Patrick alisema alikuwa anaidai kampuni hiyo Sh. milioni 1.88 ambazo ilianza kulipa kidogo kidogo mpaka Mkuu wa Mkoa alipotoa maagizo ndipo akalipwa fedha zote.

Alisema kampuni hiyo wamefanya nayo kazi kwa muda mrefu na hawakuwahi kusumbuana hali ambayo iliwafanya mwanzoni wakati hawalipwi wavumilie.

"Mimi mpaka mwisho nilikuwa namdai Sh. 452,000 ambazo amenilipa jana (juzi) baada ya maagizo ya Mkuu wa Mkoa, tunashukuru serikali kwa kutusaidia lakini tunaomba huyu mtu aendelee kununua matunda kwa sababu tumefanya naye kazi kwa muda mrefu," alisema Yusta.

Wilson Bukuku aliiomba serikali iwasaidie ruzuku ya mbolea yenye madini ya Salfa ili kuzuia ugonjwa wa fangasi ambao ndio umekuwa ukiwaathiri matunda yao na kuharibu soko.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Kilimo iliahidi kuwasaidia kama ambavyo ilifanya kwa wakulima wa korosho wa mikoa ya Lindi na Mtwara ambao pia walikuwa wamekumbwa na tatizo hilo la fangasi.



Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi, mkoani Morogoro, wakisoma nyaraka kabla ya kupitisha azimio la kumpongeza Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Khamis Katimba, kwa kuongeza ukusanyaji wa mapato, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani, mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# CWT: Wanaosababisha migogoro waadhibiwe

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) kimeiomba serikali kuwachukulia hatua za kinidhamu baadhi ya watumishi wa umma ambao wanabainika kusababisha migogoro kati ya walimu na serikali kwa kushindwa kusikiliza kero na kuzitatua.

Makamu wa Rais wa CWT, Suleiman Ikomba alitoa ombi hilo wakati akizungumza na walimu wa Halmashauri za Wilaya ya Rungwe, Busokelo na Kyela ambao walijitokeza kuwasilisha kero na malalamiko yao muda mrefu kwenye Kliniki ya Samia Teacher's Mobile ambayo ilifanyika katika Chuo cha Ualimu cha Tukuyu.

Alisema yapo baadhi ya malalamiko ya walimu yanasababishwa na uzembe wa watumishi wachache ambao hawawajibiki ipasavyo kwenye nafasi zao hali ambayo inawapunguzia walimu ufanisi wa kutekeleza majukumu yao.

Alisema matatizo hayo yanasababisha wakati mwingine walimu waichukie serikali kwa sababu ya makosa ya watumishi hao wachache na hivyo akaomba uchunguzi uwe unafanyika na kuwachukulia hatua za kiutumishi watumishi hao.

"Kuna stahiki zingine za walimu unakuta serikali ilishatoa maelekezo zitolewe kwa walimu lakini watumishi wachache wanazikwamisha kwa makusudi ama kwa uzembe tu, sasa tunaomba serikali iwe inawashughulikia ili kupunguza malalamiko haya," alisema Ikomba.

Alisema baadhi ya watumishi hao wamekuwa wakitumika kuvuruga umoja wa walimu ili washindwe kudai haki zao ambazo wanazistahili kwa mujibu wa sheria.

Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Mbeya, Nelusigwe Kajuni, alisema kliniki hiyo inafanya kazi ya kusikiliza malalamiko ya walimu na kuyatafutia majibu ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao bila kuwapo kwa vikwazo.

Alisema kliniki hiyo inawahudumia walimu ambao ni wanachama wa CWT na hata ambao siyo wanachama na hivyo akawataka walimu wote wenye malalamiko kujitokeza kwenda kuyawasilisha ili wasikilizwe na kutatuliwa shida zao.

Akizungumza na walimu hao ambao wamejitokeza kwenye Kliniki ya Samia Teacher's Mobile, Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Emmanuel Kayuni aliwashauri walimu kuandika barua kila wanapokuwa na malalamiko ili kutunza kumbukumbu.

Hivyo, aliwataka wanapowasilisha malalamiko ama shida zao kwenye mamlaka yoyote wabaki na nakala ya barua kwa ajili ya kumbukumbu ili wasipotimiziwa wawe na vielelezo.

Baadhi ya walimu waliishukuru serikali kwa kuwasogezea huduma hiyo wakidai kuwa awali walikuwa wanalazimika kwenda kuwasilisha malalamiko yao wizarani mkoani Dodoma.

## Biashara sokoni Ndanto saa 24

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Patrick Mwalunenge, ameahidi kufunga taa eneo la Soko la Ndanto Halmashauri ya Rungwe, ili kuwasaidia wajasiriamali wa eneo hilo kufanya shughuli zao usiku na mchana.

Aidha, Mwalunenge ameahidi kuwawezesha vijana 50 mbolea na mbegu ili kuwaunga mkono kwenye kilimo cha viazi mviringo msimu ujao kwa lengo la kuimarisha uchumi wao na kujiinua kiuchumi.

Aliwataka vijana wa kata hiyo kuacha vurugu na badala yake waendelee kufanya shughuli zao za kiuchumi ikiwemo kilimo na biashara ili kujiletea maendeleo pamoja na kuvutia wawekezaji ambao watasaidia kuongeza uzalishaji.

Vilevile, aliahidi kuwaunga mkono wananchi wa kata hiyo kwenye ujenzi wa kituo cha polisi ili kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama katika eneo hilo.

Baadhi ya wakazi wa kata hiyo waliiomba serikali kuwasaidia kuboresha miundombinu ya barabara katika eneo hilo ili kuwarahisishia usafirishaji wa mazao mbalimbali ikiwamo viazi ambavyo ndiyo zao kuu wanalozalisha.

Mmoja wa wananchi hao, Juhudi Mwambenja, alisema wakati wa masika wanashindwa kusafirisha mbolea, viazi kutoka shambani kwenda sokoni hali ambayo inazorotesha uzalishaji.

Alisema kutokana na hali hiyo wamekuwa wakitumia gharama kubwa kusafirisha mazao kutoka kwenye mashamba kwenda barabarani kwa kuwatafuta vibarua wa kujitwisha kichwani.



## Viongozi wakumbushwa 4R za Samia

**Na Mwandishi Wetu**

VIONGOZI kuanzia ngazi ya mkoa, wilaya, kata na vijiji Wilaya ya Tandahimba mkoani Mtwara, wametakiwa kutekeleza dhana ya 4R za Rais Samia Suluhu Hassan katika majukumu yao kwa serikali na wananchi na kuzingitia misingi ya uraia na utawala bora.

Wito huo ulitolewa juzi na Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Rashid Shabani wakati wa mafunzo hayo ya elimu ya uraia na utawala bora kwa viongozi wa Halmashauri ya Tandahimba yaliyotolewa kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya.

Shaban, alisema Wizara ya Katiba na Sheria imeweka mkakati wa kutoa mafunzo hayo kwa viongozi kuanzia ngazi ya vijiji hadi mkoa nchini kuwasaidia wananchi kufahamu sheria na kukabiliana na changamoto zinazowakabili katika jamii.

"Naomba viongozi tuliopata mafunzo haya tukayatumie kwa vitendo ili wananchi wetu wakapate elimu tuliyopewa na viongozi kutoka Wizara ya Katiba, na Sheria," alisema.

Aliishkuru wizara hiyo kwa mafunzo hayo kwa wenyeviti wa vijiji, makatibu tarafa, na madiwani kwa kuwa yatawasaidia kufahamu majukumu ya serikali kuhudumia wananchi.

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma na Sheria kwa Umma wa Wizara hiyo, Abrahiman Mshamu, alisema lengo la mafunzo hayo kwa watendaji hao ni kwenda kutoa elimu kwa wananchi ya utambuzi wa sheria mama.

Mshamu, alisema wizara hiyo imeamua kutoa mafunzo hayo katika mikoa mbalimbali nchini ili kuhakikisha kila mwanachi anashiriki kutoa maoni.

"Wizara imeweka mkakati wa kuhakikisha jamii inapata uelewa kuhusu sheria mbalimbali, hivyo imeanza kwa watendaji wa kata ili wakawe mabalozi wazuri wa utoaji elimu kwa jamii," alisema.

Mafunzo hayo yanaambatana na Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inayoendelea kutoa huduma kwa wananchi katika halmashauri za Mkoa wa Mtwara.

**Wizara imeweka mkakati wa kuhakikisha jamii inapata uelewa kuhusu sheria mbalimbali, hivyo imeanza kwa watendaji wa kata ili wakawe mabalozi wazuri wa utoaji elimu kwa jamii.**

# Wananchi wavamia hifadhi za barabara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

**Miundombinu ya barabara ni uwekezaji muhimu unaofanywa na serikali kwa maendeleo na ustawi wa wananchi.**

WANANCHI wametakiwa kuacha kuvamia maeneo ya hifadhi za barabara kwa ujenzi wa makazi na kufanya biashara kinyume cha sheria .

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Barabara Zanzibar (ZANROADS), Yasser De Costa, alitoa rai hiyo wakati wa ziara ya kukagua barabara ya Tomondo Changu hadi Mwanakwerekwe Nyumba mbili.

Costa, alisema ametoa rai hiyo baada ya kuzuka tabia ya baadhi ya wananchi kuvamia maeneo hayo kwa ujenzi wa nyumba na kuathiri barabara hizo na usalama wa maisha yao.

Alisema miundombinu ya barabara ni uwekezaji muhimu unaofanywa na serikali kwa maendeleo na ustawi wa wananchi.

"Yupo mwananchi amejenga katika eneo hili na ukizingatia anakibali, hivyo nitumie fursa hii kuutaka uongozi wa ZANROADS kukaa pamoja na mwananchi huyo kuangalia uwezekano wa kutatua tatizo hilo," alisema.

Costa, alisema uharibifu huo unaweza kusababisha hasara kubwa kiuchumi na kuchelewesha kuanza kutumika barabara.

Alisema wananchi wanapaswa kuheshimu sheria na taratibu za ujenzi ili kulinda rasilimali za umma na kuhakikisha usalama kwa sehemu zote.

Mwajuma Juma, mmoja wa wananchi waliojenga nyumba kwenye hifadhi ya barabara, alisema anahati ya miliki ya eneo hilo kwa muda mrefu na kibali cha ujenzi kutoka mamlaka husika.

Aliiomba serikali kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kufuata sheria na kuhakikisha maeneo ya hifadhi yanatumiwa ipasavyo.



Sehemu ya washiriki wa mkutano wa 98 wa wadau wa kodi wa nchi za Afrika Mashariki, wakimsikiliza Kaimu Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar, Said Ali Mohammed (hayupo pichani), wakati akifungua mkutano huo, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ACT wazungumzia kuondoa umaskini Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha ACT Wazalendo, Othman Masoud Othman, amesema Zanzibar itapiga hatua kwa kumiliki na kutumia kikamilifu vyanzo vya uchumi vilivyopo Kisiwa cha Unguja na Pemba na kuondoa umasikini kwa wananchi.

Othman aliyasema hayo kwa nyakati tofauti katika mikutano ya ndani iliyofanyika Jimbo la Tumbe, Mapofu na Wingwi yaliyopo Wilaya ya Micheweni.

Alisema hayo yatawezekana iwapo wananchi wa Unguja na Pemba wataungana kuleta mabadiliko ya nchi na uongozi wa siasa.

Alisema Wazanzibari kuamka na kuungana kukiunga mkono ACT Wazalendo ni kuitikia wito wa viongozi wa juu kutimiza dhamira ya kuisaidia Zanzibar kubadili maisha ya wananchi na kupambana na umasikini na kuleta uchumi imara.

Othman, alisema kuimarika kwa uchumi huo, kutasaidia kuzalisha ajira za heshima na mishahara ya kuwiana na kazi kwa vijana

Alisema silaha kubwa ya chama chochote cha siasa duniani ni kuleta mabadiliko na kuwa na viongozi imara na wanachama kushiriki katika uchaguzi.

Alisema hatua hiyo inakuja baada ya kujiandikisha kuwa wapiga kura na kuwachagua viongozi wenye uwezo wa kuleta maendeleo.

Othman, alisema ni lazima wananchi wa Zanzibar kuutambua mwaka huu wa uchaguzi ni muhimu kwa mabadiliko na kuutuma kuiunga mkono ACT kwa ajili ya kuleta maendeleo.

Aliwataka kujitokeza kwa wingi kutumia awamu ya mwisho ya uandikishaji katika daftari la kudumu la wapigakura litakaloanzia Wilaya ya Micheweni mwezi ujao ili kuwa na sifa ya kuchagua viongozi Oktoba mwaka huu.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama hicho, Omar Ali Shehe, alisema uchaguzi wa mwaka huu ni maalum kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kukichagua chama hicho.

Shehe, alisema ujumbe huo unapaswa kuwafikia watu wote ili waungane bila kujali uzanzibari na kuweka mbele mapenzi kwa nchi yao.

# Turufu ya Tanzania Mkutano wa Nishati

**Na Elizabeth Zaya**

TANZANIA imeweza. Hivi ndivyo unavyoweza kutamka kutokana na maandalizi yenye mafanikio makubwa ya Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika uliomalizika juzi.

Ni katika Ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa wa Mwalimu Nyerere (JNICC), ulipofanyika mkutano huo kwa siku mbili mfululizo, Januari 27 na 28, siku ya kwanza ikihusisha Mawaziri wa Wizara ya Nishati, Fedha na wakuu wa taasisi kutoka katika nchi hizo na ya pili ilikuwa ya Marais kutoka katika nchi zaidi ya 20.

Licha ya mkutano huo kufanyika kwa siku mbili, maandalizi yake yalikuwa ya kiwango cha hali ya juu kuanzia mpangilio, ulinzi na vivutio mbalimbali kwenye mitaa.

Mkutano ulivyoandaliwa na kupangiliwa, ilitosha kupeleka salamu nzuri ya Tanzania duniani.

Katika hali ya kawaida, Dar es Salaam, huwa ni mji wa pilika na 'hekaheka' nyingi zinazohusisha watu na shughuli zao nyingi ambazo wakati mwingine kutokana na kutopangiliwa vizuri huchangia uonekane una msongamano na wakati mwingine kupunguza mvuto wake halisi.

Lakini, katika siku hizo mbili za mkutano, Dar es Salaam hasa katika eneo la Posta na viunga vya karibu, lilionekana likiwa tulivu kwa kutembea kwa gari au kwa miguu ilikuwa ni raha na haichoshi kwa sababu ilikuwa ni kama sehemu ya kuburudisha macho, yakitazama majengo mazuri na masafi yakiwa hayajasongwa kwa kuegeshwa magari ovyo au wafanyabiashara wadogo kupanga bidhaa zao pembeni ya barabara na wengine kutandaza chini bila mpangilio.

Katika viunga vya karibu na ukumbi wa mkutano, Jeshi la Polisi lilijipanga, wakiwamo askari waliotumia farasi wakizunguka eneo hilo huku wageni wakiruhusiwa kuwashika wanyama hao.

Nje ya ukumbi kulikuwa na burudani za aina tofauti zote zikiwakilisha vivutio na tamaduni zilizopo Tanzania.

Katika eneo la mzunguko wa barabara ya Obama na Daraja la Tanzanite, kuliwekwa wanyama wakavu ambao nao walifanyika kama sehemu ya kutangaza vivutio vya utalii nchini na watu walishuhudiwa wakifika katika eneo hilo kufurahia.

Ukiachana na maeneo hayo ya nje, ndani ya ukumbi wa mkutano, kulikuwa na mvuto wa aina yake, kuanzia lango kuu la kuingilia, unapokewa na burudani zilizofanyika kiasili kulingana na baadhi ya nchi zilizokuwa zikishiriki katika mkutano huo.

Pia, kulikuwa na maonesho ya kitalii yaliyoshirikisha baadhi ya taasisi za Tanzania zilizopo katika sekta hizo ambazo zilitoa fursa kwa wageni kutembelea na kujifunza mambo mbalimbali, ikiwamo vivutio vilivyopo katika hifadhi tofauti za utalii za Tanzania.

**UWASILISHAJI MADA**

Hili ndilo lilikuwa la msingi zaidi na hakika lilitendewa haki, kuanzia siku ya kwanza ya mkutano iliyohusisha Mawaziri na Wakuu wa taasisi na hata siku ya pili ambayo ndiyo ilikuwa ya kuhitimisha.

Vyombo vya habari vya Tanzania na vya mataifa mbalimbali vilivyoshiriki katika mkutano huo, vilifanya kazi kwa uhuru huku nyenzo zote za kumwezesha mwandishi wa habari zikiwa zimewekwa katika mpangilio maalumu ambao haukuathiri utekelezaji wa majukumu ya vyombo hivyo.

Baadhi ya waandishi wa habari kutoka mataifa ya nje, walishuhudia hilo, baadhi wakisema miongoni mwa mikutano ya kimataifa waliyowahi kuhudhuria katika mataifa mengine, huo wa Tanzania ni miongoni mwa ambayo imefanyika na kupangiliwa kwa ubora wa hali ya juu.

Si tu waandishi hao wa habari wa kimataifa waliyoipongeza Tanzania kwa mkutano huo mzuri, lakini hata baadhi ya mawaziri na marais katika sehemu ya uwasilishaji wa mada zao katika mkutano huo, walilitamka hilo kwa uwazi huku wakimpongeza kiongozi namba moja wa taifa hili, Rais Samia Suluhu Hassan kwa maandalizi mazuri.

Mkutano huo wa nishati umevunja rekodi ya kuhudhuriwa na marais wengi zaidi kwa wakati mmoja nchini, ukiacha tukio la mazishi ya aliyekuwa baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere mwaka 1999 na ule wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), uliofanyika mwaka 2019 ambao ulihudhuriwa na wakuu wa nchi 15.

Kumbukumbu nzuri nyingine ambayo marais hao wameondoka nayo na kukiri ni Tanzania ilivyofanikiwa kusambaza umeme kwa wananchi wake mpaka vijijini wakisema inapaswa kuwa mfano wa kuigwa.

Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Ulaya (UN), Amina Mohamed, aliipongeza Tanzania kwa kupanua huduma ya upatikanaji wa umeme na kuweka nguvu kwenye uwekezaji wa nishati mbadala akisema hilo ni miongoni mwa mambo yanayochochea uchumi.

Mwingine aliyeipongeza Tanzania kwa kufanikisha umeme vijijini ni Rais wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Dk. Akinumwi Adesina, aliyesema kwamba hatua iliyofikia Tanzania inachangia maendeleo na ustawi wa wananchi vijijini.

Kwa mujibu wa Rais Samia, katika usambazaji umeme, mpaka sasa Tanzania imefikia vitongoji 32,827 na mwelekeo ni kuvifikia vitongoji 64,359.

Katika mkutano huo, wakuu wa nchi hizo waliwasilisha na kuridhia Azimio la Dar es Salaam la kuhakikisha zinafikisha umeme kwa wananchi milioni 300(mission 300) ifikapo mwaka 2030, ambalo pamoja na mambo mengine linasisitiza kusambaza nishati ya uhakika kwa gharama nafuu, kuhamasisha matumizi ya nishati safi na kuimarisha miundombinu.



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba (kulia), akifurahia jambo na Rais wa Benki ya Dunia, Ajay Banga, wakati alipomsindikiza katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam jana. Banga, alikuwa nchini kuhudhuria Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Afrika, uliomalizika juzi. **PICHA: WF**

# TCCIA walia utitiri wa kodi kuwakwamisha

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

CHEMBA ya Wafanyabiashara wa Viwanda na Kilimo (TCCIA), Mkoa wa Morogoro imesema utitiri wa kodi unaotozwa na taasisi tofauti za serikali umekuwa ni sehemu ya kukwamisha juhudi za wafanyabiashara katika mkoa huo kuleta maendeleo na kukuza uchumi

Akichangia kutoa maoni kwa wajumbe wa Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi, Mwenyekiti wa Chemba ya TCCIA, Mkoa wa Morogoro, Mwadhine Mnyanza, alisema wafanyabiashara wanakumbana na changamoto hizo na kumuomba Rais Samia Suluhu Hassan,kuangalia uwezekano wa kupunguza wingi wa kodi ambao umekuwa kikwazo kwao.

Aidha, alitaja eneo lingine ni suala la kodi kubwa hasa kwenye sekta za kibiashara jambo ambalo linasababisha baadhi ya wafanyabiashara kufikia hatua ya kukwepa kodi.

Mfanyabiashara Redempta Mushi alisema kuwa zipo changamoto kwa wanaofanya biashara zao upande wa pili wa Muungano (Zanzibar).

Mushi alisema mfanyabiashara kutoka Tanzania Bara anatakiwa alipe kodi anapopeleka biashara zake Zanzibar, lakini mfanyabiashara kutoka Zanzibar halipi kodi jambo ambalo inafaa liangaliwe upya ili kuweka uwiano kwa pande hizo mbili.

Meneja wa Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO), Mkoa wa Morogoro, Joan Nagawe, alisema kuwa elimu ya kodi bado ni changamoto kwa watu wengi kwa sababu mfumo uliopo wa elimu ya Tanzania haujumishi elimu ya kodi kuanzia shule ya awali na msingi.

"Ombi langu ni kwamba Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi wakati mtakapo wasilisha haya mapendekezo jambo hilo la kuwepo kwa mfumo wa elimu ya kodi kuanzia shule ya awali liwepo," alisema Nagawa.

Alisema elimu ya kodi itolewe kuanzia kwa watoto wadogo, shule ya msingi na sekondari ili wanapotoka wajue umuhimu wa kodi kwa maendeleo ya taifa.

Katibu Tawala Msaidizi Sehemu ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mkoani Morogoro, Beatrice Njawa, alisema ni muhimu kuangalia namna ya kuboresha mazingira ya biashara nchini na eneo moja la kodi ambalo linaweza kuwavutia wawekezaji wengi.

Njawa aliiomba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kushirikiana na taasisi nyingine katika suala la kutoa mafunzo na elimu kwa wafanyabiashara kutambua umuhimu wa kulipa kodi.

Kamishna wa Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi, Balozi Mwanaidi Maajar, aliwataka wafanyabiashara na wadau mbalimbali wa kodi mkoani Morogoro kutoa maoni ya kero na changamoto na mapendekezo kwa kuyaweka kimaandishi na kuyatuma kwa barua pepe katika sektretarieti yatumie hiyo ili yafanyiwe kazi ya utekelezaji.

"Nazipongeza halmashauri zote zilizofika kwenye kikao hiki, wafanyabiashara na wadau mbalimbali wa kodi sisi wajumbe tutaweka maoni yetu, lakini hamwajibiki kujibu hapa, tunaziweka hapa ili mtakapoleta maandiko yenu muweze kuyaboresha au mrekebishe pale ambapo tumeuliza maswali kwa ajili ya ufafanuzi kwenye jambo fulani," alisema.

Balozi Maajar ambaye pia ni mshauri wa masuala ya sheria, alisema kuwa changamoto waliyokutana nayo katika maeneo waliyopita suala la utiriri wa kodi na watozaji wenyewe na jambo hilo limejirudia mara nyingi.

"Huko tulikopita pia tumekutana na malalamiko haya na wametueleza wanafika watozaji watano kwa siku moja kwa wiki bila mtu kujua na pia kodi nyingine zinajirudia," alisema.

Balozi Maajar alitoa mfano wa utozaji kodi wa mpunga pamoja na kodi ya mchele jambo ambalo kimsingi limelalamikiwa na wafanyaashara kwenye halmashauri zenye uzalishaji wa zao hilo.

"Mfano unaweza kuchukua mchele Dakawa, Wilaya ya Mvomero unalipa kodi, ukija nao Wilaya ya Kilombero unalipa kodi," alisema Balozi Maajar.

**Katika hatua nyingine, Rais wa Tanzania ambaye ni Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC-Organ), Samia Suluhu Hassan, aliongoza mkutano wa dharura wa wakuu wa nchi na serikali wa asasi hiyo uliofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam.**




Sehemu ya wakazi wa Goma mashariki mwa DRC waliopoteza makazi yao na kupata hifadhi nchini Rwanda, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Wananchi 100 wauawa Goma, washauri vijana kubeba silaha

## • Hospitali zazidiwa kwa majeruhi

**Na Maulid Mmbaga**

MILIO ya mabomu na mitutu ya risasi imeendelea kusikika katikati mwa mji wa Goma ulioko mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) baada ya waasi wa M23 wanaodaiwa kuungwa mkono na Rwanda kuendelea kusonga mbele, machafuko ambayo yamesababisha zaidi ya watu 100 kuuawa.

Ikiwa ni siku ya tatu tangu mapigano yashamiri katika mji huo, AFP inayonukuu takwimu za hospitali za mitaa huko Goma, inasema vita hivyo vimesababisha pia majeruhi kwa zaidi ya wananchi 1,000, huku makazi yakiharibiwa pamoja na kuathiri upatikanaji wa huduma za kijamii kama chakula, umeme na maji.

Kamati ya kimataifa ya Msalaba Mwekundu, inasema hali hiyo iliwalazimu wafanyakazi wake kugeuza maegesho ya magari ya hospitali kuwa kitengo cha kufanya tathmini ya awali ya wagonjwa au majeruhi.

Inaeleza kuwa kitendo cha kutumia silaha nzito za kivita katika maeneo yenye watu wengi husababisha majeraha makubwa, haswa miongoni mwa watoto.

Kutokana na machafuko hayo, umati wa watu wenye hasira huko mjini Kinshasa uliandamana barabarani na kuchoma magurudumu ya pamoja na kushambulia balozi za mataifa mbalimbali ikiwamo Rwanda, Ufaransa, Ubelgiji, Marekani, Kenya, Uganda na Afrika Kusini.

Pamoja na vifo vya raia, Afrika Kusini inasema kwamba wanajeshi wake wengine wanne, ambao wako DRC kama sehemu ya juhudi za kulinda amani, walikufa kutokana na mapigano na M23.

Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa alizungumza na mwenzake wa Rwanda Paul Kagame, huku wawili hao wakikubaliana kuhusu hitaji la dharura la kusitishwa kwa mapigano na kuanzishwa tena kwa mazungumzo ya amani.

Pia inaelezwa kuwa mashambulizi ya M23 yamesababisha mgogoro mkubwa wa kibinadamu katika mji huo, huku Umoja wa Mataifa (UN) ukionya juu ya uwezekano wa watu wengi kuhama makazi yao, wakishuhudia uhaba mkubwa wa chakula, hospitali zikielemewa na majeruhi pamoja na kuenea kwa milipuko ya magonjwa.

Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu (ICRC), Myriam Favier anasema makombora yanarushwa juu ya nyumba za wananchi huku wapiganaji wakifyatua silaha nzito katikati mwa jiji la Goma "Ni eneo lenye watu wengi ... waathiriwa ni wengi upande wa raia".

Anasema licha ya vurugu hizo, maduka kadhaa huko Nyiragongo, eneo la kaskazini mwa Goma, yalifunguliwa kwa saa chache. "Hiyo iliruhusu watu kununua chakula, lakini tangu kuongezeka kwa vurugu hakujakuwa na umeme, hali inayoashiria kuwa hakuna maji katika jiji pia".

### VIJANA BEBENI SILAHA

Kutokana na kinachoendelea Goma viongozi wakuu wa serikali nchini DRC wametoa wito wa usajili wa kizalendo na kuwahimiza vijana kujiandikisha katika jeshi, huku M23 wakiendelea na mashambulizi katika mji huo.

Waziri wa Mipango, Guy Loando Mboyo amezindua kampeni iliyopewa jina la (Tuchukue hatua kwa ajili ya nchi yetu, tunakataa vita), kwa matumaini ya kuwashawishi watu kujiunga.

Pia Waziri wa Uchukuzi, Jean Pierre Bemba ambaye yeye mwenyewe ni kiongozi wa zamani wa waasi alinukuliwa akisema atataka kila mkoa wa nchi hiyo kusajili vijana 20,000 kupigana na jeshi.

Wakati hamasa hiyo ikiendelea inaelezwa kuwa waasi wa M23 wanaoungwa mkono na Rwanda wameendelea kuimarisha udhibiti wao dhidi ya mji wa Goma. Huku vijana wakiingia mitaani huko Kinshasa wakilaani kutochukuliwa hatua za kimataifa vita hivyo ambako walishambulia balozi za Ubelgiji, Ufaransa, Kenya, Afrika Kusini, Marekani na Uganda.

Serikali ya Kenya inasisitiza Kongo kuchukua hatua za haraka kurejesha utulivu na kulinda balozi zao za kidiplomasia.

Hata hivyo, Umoja wa Afrika (AU) umelaani machafuko hayo na kuwataka M23 waweke silaha chini. Huku Baraza la Amani na Usalama la AU likifanya kikao cha dharura cha mawaziri jana kujadili mgogoro huo.

Pia Jeshi la kulinda amani la Umoja wa Mataifa mashariki mwa DRC (MONUSCO) pia limeonya juu ya hatari ya kuzuka mashambulizi ya kikabila huku hali ikizorota katika eneo hilo.

Naibu mwakilishi maalum wa operesheni za MONUSCO, Vivian van de Perre anasema mashambulizi ya kikabila katika eneo hilo yanapaswa kuchukuliwa kwa umuhimu mkubwa.

De Perre amesema MONUSCO imepokea idadi kubwa ya watu wanaotafuta hifadhi, wakiwamo maofisa na wapiganaji au askari waliosalimisha silaha zao. Na kwamba kuna uhaba mkubwa wa maji, chakula na vifaa vya matibabu.

### HATUA ZA MAREKANI

Ubalozi wa Marekani umewaambia raia wake waondoke nchini humo kutokana na mashambulizi hayo huku Mkuu wa Sera za Kigeni wa Umoja wa Ulaya, Kaja Kallas akisema vitendo vya mashambulizi havikubaliki na vinazua wasiwasi mkubwa.

Waziri wa Mambo ya Nje wa DRC, Therese Wagner, anasema Kongo inaheshimu kanuni zinazosimamia uhusiano wa kidiplomasia, na kwamba serikali imechukua hatua zote muhimu kuhakikisha ulinzi wa balozi zilizoidhinishwa nchini humo.

Inaelezwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Marco Rubio, anasema Marekani ina wasi wasi kutokana na mzozo unaoendelea, na hasa kuanguka kwa mji wa Goma mikononi mwa waasi wa M23, huku akisisitiza mapigano kusitishwa mara moja kwenye eneo hilo na kwamba pande zote ziheshimu uhuru wa kieneo.

### SHINIKIZO LA KIMATAIFA

Katika ishara ya shinikizo linaloongezeka dhidi ya Kigali, Ujerumani imeufuta mkutano uliopangwa na maofisa wa Rwanda, ikishutumu ukiukaji wa wazi wa sheria za kimataifa.

Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ya Shirikisho la Ujerumani (BMZ) imefutilia mbali mkutano huo uliopangwa kufanyika mwezi wa Februari, mwaka huu.

Msemaji wa wizara hiyo anasema kutokana na hali ya sasa ya kuongezeka mgogoro, mambo hayawezi kuendelea kama kawaida, na kwamba mazungumzo yanaweza kuanza tena wakati Rwanda na M23 zitakapoacha kuendeleza mzozo huo na kuondoka.

Kadhalika inaelezwa kuwa kutokana na mji wa Goma kuwa karibu na miji ya uchimbaji madini yenye utajiri wa dhahabu, bati, na coltan ambayo ni muhimu kwa simu za rununu na betri za magari ya umeme, imechangia kuongezeka kwa mzozo unaoendelea.

Katika hatua nyingine, Rais wa Tanzania ambaye ni Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC-Organ), Samia Suluhu Hassan, aliongoza mkutano wa dharura wa wakuu wa nchi na serikali wa asasi hiyo uliofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam.

Katika mkutano huo, Rais Samia alishiriki pamoja na Rais wa Jamhuri ya Zambia, Hakainde Hichilema, pamoja Rais wa Malawi, Dk. Lazarus Chakwera huku Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa na Rais wa DRC Felix Tshisekedi wakishiriki kwa njia ya mtandao.

**Chanzo Mtandao**

HABARI MICHEZO

# TABORA UNITED FC YARUSHA 'KIJEMBE' IKIWAALIKA SIMBA

**Na Faustine Feliciane**

ZIKIWA zimesalia siku tatu kabla ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba, uongozi wa Tabora United umetupa kijembe kwa Wekundu wa Msimbazi wakiwataka kutafuta visingizio mapema kwa sababu mchezo huo watapoteza.

Tabora United itawakaribisha Simba katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani, Tabora.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Agosti 18, mwaka jana, Simba iliwachapa Tabora United mabao 3-0, hapo ilikuwa bado haijapata makali.

Ofisa Habari wa Tabora United, Christina Mwagala, alisema wamejiandaa vizuri kuikabili Simba na kuwataka kutafuta kabisa 'visingizio' watakavyojitetea baada ya kupoteza mchezo huo.

Mwagala alisema wataendelea kutoa dozi kwa timu zote zinazojiona ni 'kubwa' katika Ligi Kuu Tanzania Bara na uwezo wa kufanya hivyo wanao.

"Tunawakaribisha sana Simba, Tabora, tumejiandaa na hakuna shaka tutaendelea kutoa dozi, watafute kabisa visingizio, hatutawaacha salama kwenye uwanja wetu wa nyumbani," alisema Mwagala.

Aliongeza anafahamu mchezo huo hautakuwa mwepesi lakini kucheza kwenye uwanja wao wa nyumbani kunawapa kila sababu ya kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

"Tunaiheshimu Simba, wana wachezaji wazuri na kwa sasa wanaongoza ligi, lakini hiyo sio sababu ya sisi kutopata ushindi kwenye mchezo wetu dhidi yao, tupo tayari kuwakabili, uwanja wetu ni mzuri na wasijiangushe, wacheze mpira," Mwagala alisema.

Mchezo huo wa mzunguko wa pili Ligi Kuu Tanzania Bara unasubiriwa kwa hamu na mashabiki wa soka hapa nchini kufuatia Tabora United kutoa vichapo kwa Yanga na Azam FC.

Timu hizo zinakutana huku Simba ikiwa kinara katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 40 baada ya kucheza michezo 15 huku Tabora United ikiwa katika nafasi ya tano kwa kukusanya pointi 25 katika michezo 15 iliyocheza.

Simba itashuka katika mechi hiyo ikiwa na kumbukumbu ya kumaliza kibabe mechi za hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika na kutinga hatua ya makundi pamoja na kupata ushindi mnono wa mabao 6-0 dhidi ya Kilimanjaro Wonders, ilipokutana kwenye mchezo wa Kombe la FA.




Wachezaji wa Yanga Princess wakishangilia bao katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Alliance Girls huku wakionyesha jezi ya mshambuliaji wa timu hiyo, Arieth Adong, ambaye kwa sasa ni majeruhi. Yanga Princess ilipata ushindi wa mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

# KMC, Azam mechi ya kisasi

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC imesema inajiandaa kulipa kisasi katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Azam FC itakayochezwa Februari 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, imeelezwa.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza msimu huu, Azam FC ilipata ushindi wa mabao 4-0.

Ofisa Habari wa KMC, Khalid Chukuchuku, alisema maandalizi wanayofanya ni maalum kwa ajili ya mechi hiyo ambayo wamejipanga kuondoka na ushindi na si matokeo mengine.

"Kwetu huu ni mchezo mkubwa, kwanza tunauheshimu kama ni moja kati ya michezo migumu katika ligi, unapokutana na Azam ujue unacheza na timu ambayo inapigania moja kwa moja kutwaa taji la Ligi Kuu, hivyo maandalizi yake yanatakiwa yawe mara nyingi zaidi ya vile ambavyo tunajiandaa kucheza na timu za madaraja yetu," alisema Chukuchuku.

Aliongeza kinachowafanya wajiandae kikamilifu ni kwenda kulipiza kisasi kwa sababu mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Septemba 19, mwaka jana wakiwa wenyeji walipoteza.

"Kwa maana hiyo tunakwenda kwenye huu mchezo tukiwa tumejiandaa kisawasawa, tunajua wana wachezaji wazuri na kocha bora, lakini haitupi sisi sababu ya kutowafunga, sasa huu ni mchezo wa kisasi, walitufunga kwenye uwanja wetu na sisi tutakwenda kuwaangusha kwao, hili linawezekana kwa sababu huu ni mpira wa miguu, kuna timu nyingi zimeshinda ugenini na kufungwa nyumbani," Chukuchuku aliongeza.

KMC inakwenda kucheza mchezo huo ikiwa kwenye nafasi ya 10 ya msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi 19, ikicheza michezo 16, ushindi michezo mitano, sare nne, ikipoteza saba.

## Maumivu ya mguu yamsumbua Awesu

**Na Somoe Ng'itu**

KIUNGO mshambuliaji wa Simba, Awesu Awesu, amesema bado anasumbuliwa na maumivu ya mguu na ndio sababu ilipelekea akae nje katika mechi ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Kilimanjaro Wonders FC kutoka mkoani Kilimanjaro.

Katika mechi hiyo ambayo Simba ilitumia wachezaji wa kikosi cha pili ilimalizika kwa Wekundu hao kupata ushindi wa mabao 6-0.

Awesu aliliambia gazeti hili anaendelea na matibabu na huenda akarejea kwenye mazoezi ya pamoja na wachezaji wenzake mwishoni mwa wiki.

"Ninasumbuliwa na maumivu katika mguu, mwalimu alinipanga ili kuona kama naweza kurejea uwanjani kamili lakini nikaumia na kushindwa kuendelea, lakini mechi dhidi ya Kilimanjaro Wonders ilikuwa nzuri, wapinzani walikuwa wanajaribu kutudhibiti kwa kiasi fulani ila tuliwashinda na uzoefu uliwaangusha," alisema Awesu ambaye alitua Simba akitokea KMC FC.

Kwa sasa Simba inaendelea kujifua kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Tabora United itakayochezwa Februari 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora.

## Dodoma Jiji yaenda kujichimbia Arusha

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Dodoma Jiji kimeenda jijini Arusha kwa ajili ya kuweka kambi ili kujiandaa na mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa imepanga kucheza mechi mbalimbali za kirafiki.

Ofisa Habari wa Dodoma Jiji, Moses Mpunga, alisema kikosi hicho kilifika Arusha juzi usiku, ambapo kitaanza mazoezi rasmi chini ya Kocha Mkuu, Mecky Maxime kwa ajili ya kuikaribisha Pamba Jiji Februari 5, mwaka huu.

"Tulikuwa na mapumziko marefu kidogo, lakini kwa sasa kikosi kimerejea katika uwanja wa mazoezi, tutacheza na timu ya TMA na Mbuni FC, zinazoshiriki Ligi ya Championship pamoja na michezo mingine ya kiushindani ambayo tumefanikiwa kuipata, lengo ni kurudi kwenye Ligi Kuu kwa kishindo, lengo letu msimu huu ni kumaliza ligi tukiwa katika nafasi nne za juu," alisema Mpunga.

Aliongeza wameridhika na usajili wa nyota wapya wawili ambao ni Abdi Banda na Muhsin Issa, wataongeza nguvu katika kikosi chao.

"Tumefanya usajili wa wachezaji wawili tu kwenye dirisha hili, Banda na Muhsin, hawa wote ni mabeki wa kati, sehemu ambayo ilikuwa inatupa changamoto katika mzunguko wa kwanza, tuliruhusu mabao mengi kutokana na kutokuwa sawa kwenye eneo la ulinzi, kocha akatupa mapendekezo yake tukayafanyia kazi," Mpunga alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CASEMIRO ATAKIWA ROMA
AS Roma inataka kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United na Brazil, Casemiro mwenye umri wa miaka 32, kwa mkopo hadi mwisho wa msimu huu, lakini uhamisho unategemea kumuuza mchezaji wa kimataifa wa Argentina, Leandro Paredes (30). (***Mail***)

### NAPOLI, JUVE VITANI
NAPOLI na Juventus zinamfuatilia mshambuliaji wa Manchester United, Rasmus Hojlund, mwenye umri wa miaka 21, huku mshambuliaji huyo wa Denmark akiwa bado hajamvutia kocha mpya, Ruben Amorim. (***Sportsport)***

### SALAH KUMRITHI NEYMAR
Al-Hilal wamepewa nafasi kubwa ya kumsajili winga wa Liverpool kutoka Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 32 msimu huu baada ya timu hiyo ya Saudi Pro League kusitisha mkataba na fowadi wa Brazil, Neymar (32). (***Telegraph)***

### CUNHA AGOMBEWA EPL
KLABU ya Wolves inatarajia ofa moja au zaidi kwa fowadi wa Brazil, Matheus Cunha, kabla ya tarehe ya mwisho ya dirisha la uhamisho, huku Aston Villa, Arsenal na Nottingham Forest wakimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Football Insider)***

### DORGU AKARIBIA UNITED
KLABU ya Manchester United inakaribia kumsajili winga wa Lecce na Timu ya Taifa ya Denmark, Patrick Dorgu, mwenye umri wa miaka 20, kwa ada ya pauni milioni 30. (***Sky Sports)***

### RASHFORD AJIIMARISHA
MSHAMBULIAJI wa Manchester United, Marcus Rashford, mwenye umri wa miaka 27, amemwajiri kaka yake ambaye ni straika wa Brighton, Danny Welbeck kama wakala wake mpya ili kumsaidia kupata uhamisho kutoka Old Trafford. (***Star)***

### TEL KUONDOKA CHELSEA
MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich na Ufaransa, Mathys Tel mwenye umri wa miaka 19, anataka kuondoka katika klabu hiyo mwezi huu na Chelsea ipo katika mazungumzo na timu hiyo ya Bundesliga. (***Mail***)


### TEL KUMRITHI RASHFORD
KLABU ya Manchester United pia itaingia kwenye kinyang'anyiro cha kumwania Mathys Tel, lakini iwapo tu Marcus Rashford au winga wa Argentina, Alejandro Garnacho mwenye umri wa miaka 20 atauzwa. (***Florian Plettenberg)***

### CITY: MC TEE HAUZWI
KIUNGO wa kati wa Manchester City, James McAtee, mwenye umri wa miaka 22, hauzwi tena na Bayer Leverkusen, huku klabu hiyo ya Bundesliga ikipanga kumsajili mchezaji wa Argentina, Emiliano Buendia (28), kutoka Aston Villa. (***Florian Plettenberg***)

### CAMBIASO AGEUKA LULU
KLABU ya Manchester City inakabiliwa na kinyang'anyiro cha kuwania saini ya Andrea Cambiaso, mwenye umri wa miaka 24. (***Nipe Sport***)

### BAYERN, UNITED VITANI
KLABU ya Bayern Munich na Manchester United zimeonyesha nia ya kumnunua mshambuliaji wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 27, ambaye thamani yake ni takribani pauni milioni 7m. (***Mail)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SAUDIA WAMWANDALIA DAU NONO VINICIUS JR

**RIYADH,** Saudi Arabia

### Kuondoka kwa Neymar kunatajwa kutarahisisha usajili huo...

WINGA wa Real Madrid, Vinicius Junior, anaendelea kuhusishwa na nia ya klabu za kutoka Saudi Arabia, huku ripoti mpya ya ofa ya rekodi ya dunia ikiandaliwa kwa kipindi cha majira ya joto.

**Vinicius amefanya vizuri na kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi duniani tangu Madrid ilipokubali dili kwa mara ya kwanza na Flamengo kwa ajili ya nyota huyo aliyekuwa na umri wa miaka 16 mwaka 2017.**

Hajashinda Ballon d'Or 2024, lakini ameshinda tuzo ya Mchezaji Bora wa FIFA wa Wanaume miezi michache baadaye.

Mchezaji huyo ameahidi mara kwa mara utii wake kwa Madrid, lakini hilo linaweza kujaribiwa na mkataba wenye faida kubwa ya fedha.

Cha ajabu, klabu halisi bado haijajulikana, lakini mfuko wa uwekezaji wa Saudia unamiliki timu nne za Ligi Kuu ambazo ni Al Hilal, Al Nassr, Al Ahli na Al Ittihad.

Al Hilal linaweza kuwa chaguo la wazi la mapema, kwa sababu Neymar sasa ameondoka kwenye klabu hiyo.

AS imeandika maofisa wa Saudi Arabia wanataka kujaribu uamuzi wa Madrid kwa ofa ya euro milioni 300, ambayo inazidi kwa mbali rekodi iliyopo ya dunia ya Euro milioni 222 iliyowekwa na Neymar alipojiunga na Paris Saint-Germain mwaka 2017.

Ni kiasi sawa na hicho kilichotolewa kwa PSG kwa Kylian Mbappe katika majira ya joto ya 2023, huku ofa hiyo ikikataliwa.

Mshahara wa jumla uliopendekezwa katika kipindi cha mkataba wa miaka mitano utafikia euro bilioni moja, sawa na euro milioni 200 kila msimu.

# ARSENAL YASHINDA RUFANI YA KADI NYEKUNDU




**LONDON,** England

KIUNGO wa kati wa Arsenal, Myles Lewis-Skelly hatatumikia adhabu ya kufungiwa mechi tatu baada ya klabu hiyo kuipinga kadi nyekundu aliyopewa kwenye mchezo dhidi ya Wolves, kukubaliwa na Tume ya Nidhamu ya Chama cha Soka cha England (FA).

Lewis-Skelly alitolewa nje kwa kadi nyekundu na mwamuzi, Michael Oliver, dakika ya 43 mechi ya ushindi wa 1-0 wa Washikabunduki hao dhidi ya Wolves iliyochezwa Jumamosi iliyopita, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 akidaiwa kumchezea rafu, Matt Doherty.

Uamuzi wa Oliver uliungwa mkono na mwamuzi wa VAR, Darren England.

Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta alisema "nimekasirishwa kabisa" na kadi nyekundu ya Lewis-Skelly, jambo ambalo lingemfanya akose mechi ya Jumapili ya nyumbani dhidi ya Aston Villa kwenye Ligi Kuu England, mchezo wa pili wa nusu fainali ya Kombe la Carabao dhidi ya Newcastle United Februari 5 na mechi ya ugenini dhidi ya Leicester City Februari 15, mwaka huu.

Ni mara ya tatu msimu huu kwa mchezaji kushinda rufani dhidi ya kadi nyekundu kwenye Ligi Kuu, licha ya VAR kuikubali.

Mnamo Septemba, nahodha wa Manchester United, Bruno Fernandes, alipewa kadi nyekundu dhidi ya Tottenham Hotspur. Kisha mnamo Novemba, nahodha wa Brentford Christian, Nørgaard alitolewa nje kwa msaada wa VAR kutokana na kumchezea vibaya kipa wa Everton, Jordan Pickford.

United na Brentford walifanikiwa kukata rufaa kwa kadi nyekundu kwa FA, huku jopo la wachezaji watatu wa zamani wakikutana kupiga kura juu ya uamuzi wa mwamuzi.

# Slot amtaja Klopp mafanikio yake

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Mkuu wa Liverpool, Arne Slot anaamini kufanana katika mtindo wake wa uchezaji na ule wa Jurgen Klopp kumemsaidia kuzoea haraka soka la Uingereza.

Timu ya Slot kwa sasa ipo mbele kwa pointi sita kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England na tayari imejihakikishia kufuzu moja kwa moja hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kabla ya mechi za mwisho zilizochezwa jana.

Akitafakari juu ya kile ambacho kimeisaidia timu yake kufikia nafasi hiyo ya uongozi, Slot alisema: "Jinsi ninavyofanya kazi ndivyo ninavyofikiria ni jinsi gani naweza kuleta mtindo wangu wa uchezaji haraka iwezekanavyo nikiwa na timu hii.

"Sababu ambayo inafanya mambo kuwa rahisi ni kuwa na ufanano wa staili ya uchezaji na ile ya Jurgen Klopp.

"Hilo ndilo jambo la kwanza. Kama kikundi, nina furaha kuwa katika nafasi tuliyo nayo. Shukrani kwa muundo mpya wa Ligi ya Mabingwa Ulaya."

Slot aliongeza: "Ilinichukua muda kuelewa muundo huu, lakini sasa ninaweza kuwa na uhakika asilimia 100, nasema ni mzuri."



# United yakaribia kumnasa Dorgu

**MANCHESTER,** England



MANCHESTER United inaendelea kufanyia kazi mpango wa kumnunua, Patrick Dorgu, kabla ya tarehe ya mwisho ya usajili wa majira haya ya baridi, kwa mujibu wa ESPN.

Lecce tayari imekataa ofa ya euro milioni 20 pamoja na nyongeza ya euro milioni tano kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark mwenye umri wa miaka 20.

Vyanzo vimeiambia ESPN, mazungumzo kati ya klabu hizo mbili yanaendelea na kuna imani inayoongezeka ofa ya euro milioni 40 inaweza kukubaliwa.

Kocha wa United, Ruben Amorim, ameonyesha nia ya kuongeza beki wa kushoto kwenye kikosi chake Januari hii, na kwa mujibu wa ripoti United pia wanaangalia uwezekano wa kuanzisha chaguo lao la kumnunua tena Álvaro Fernández kutoka Benfica kwa dau la euro milioni 18.

Mhitimu huyo wa zamani wa akademi ya Old Trafford, ambaye amefanya vyema nchini Ureno, anachukuliwa kuwa chaguo la pili kama dili la Dorgu halitakubaliwa.

Iwapo Dorgu au Fernandez watawasili, United itasikiliza ofa za mkopo kwa Tyrell Malacia.

Kuna matumaini, Luke Shaw anakaribia kurejea kutokana na jeraha.

Vyanzo pia vimeiambia ESPN, United itasikiliza ofa za mkopo kwa Casemiro kabla ya tarehe ya mwisho hapo Jumatatu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil ameanza mchezo mmoja tu kati ya 11 zilizopita na amekuwa mchezaji wa akiba ambaye hajatumiwa katika mechi sita zilizopita.

Mechi yake ya mwisho ilikuwa katika kichapo cha 2-0 kutoka kwa Newcastle United Desemba 30, mwaka jana.

Roma imeonyesha nia ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 hadi mwisho wa msimu.

Vyanzo vimeiambia ESPN, United iko tayari kulipa sehemu ya mshahara ya Casemiro, ambao ni zaidi ya pauni 300,000 kwa wiki.

## Azik Ki, Mzize rasmi sokoni

INATOKA UKURASA 24

Yanga ilitolewa katika michuano inayosimamiwa na Shirikisko la Soka Afrika (CAF), baada ya kukubali kulazimishwa sare ya bila kufungana dhidi ya MC Alger na kumaliza nafasi ya tatu kwenye Kundi A lililoongozwa na Al Hilal ya Sudan.

Katika hatua nyingine, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amewaonya wachezaji wake kutofikiria chochote juu ya kutinga robo fainali ya Kombe la FA baada ya kupata ushindi mnono wa mabao 6-0 dhidi ya Kilimanjaro Wonders, na kuimarisha mipango yao kwa lengo la kusaka pointi tatu ikiwafuata Tabora United.

Fadlu amewaambia pia wachezaji wake 'wasivimbe vifua' na kujiamini baada ya kuifunga CS Constantine ya Algeria mabao 2-0 na kutinga robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika na kuamini wanaweza kuifunga Tabora United kirahisi.

"Nimezungumza na vijana wangu tunakwenda kuianza duru ya pili ya Ligi Kuu, ili kuwa mabingwa tunawajibika kushinda kila mchezo ambao upo mbele yetu, tunapaswa kushinda mchezo dhidi ya Tabora pamoja na ugumu wake, kwa maana Tabora hii siyo ile tuliyoifunga katika mzunguko wa kwanza," alisema kocha huyo.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema kikosi chao kinaendelea vyema na maandalizi, huku kukiwa na habari njema ya kuhusiana na mchezaji wao, Awesu Awesu.

Aliongeza kikosi chao kitaondoka jijini kuelekea mkoani Tabora keshokutwa na wanafahamu mchezo huo wa Jumapili utakuwa mgumu kutokana na ubora wa sasa wa Tabora United, lakini wana imani wataibuka na ushindi.

"Kwanza lazima tukiri Tabora United ni timu nzuri na imeimarika sana ingawa ilianza msimu vibaya, timu hii imepata kujiamini baada ya kuzifunga timu kubwa ikiwamo Yanga (mabao 3-1), na baadaye Azam (mabao 2-1) ambazo ni timu kubwa, ndiyo maana inaamini pia inaweza kufanikiwa kutufunga na sisi.

Tunawaambia kitu kimoja, ni kweli imezishinda timu ambazo zinakaribiana na sisi, lakini sisi siyo wao," alitamba Ahmed.

# SIMBA QUEENS, SHIKANGWA HAWASHIKIKI LIGI WANAWAKE

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba Queens inaendelea kujiimarisha katika msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), mshambuliaji wa timu hiyo, Jentrix Shikangwa, amefunga hat trick ya tatu msimu huu katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Manyara juzi.

Mechi hiyo ilimalizika kwa wenyeji kuchapwa mabao 4-2, licha ya kutangulia kufunga mabao mawili kabla ya Simba kusawazisha na kupachika mengine mawili yaliyowapa pointi tatu muhimu.

Kwa matokeo hayo, mabingwa watetezi, Simba Queens imefikisha pointi 28 na kuendelea kuongoza katika msimamo wa ligi hiyo ikifuatiwa na JKT Queens yenye pointi 26, lakini ikiwa na mchezo mmoja mkononi.



Jentrix sasa amefikisha mabao 16 na kuwa kinara katika orodha ya wafungaji akichuana kwa karibu na Stumai Abdallah wa JKT Queens ambaye juzi alifunga bao moja katika ushindi wa magoli 3-0 dhidi ya Bunda Queens.

Bao lingine la Simba Queens katika mchezo huo lilifungwa na kiungo Mkenya Vivianne Corazone wakati Amina Hemedi na Mariam Elia, waliifungia Fountain Gate Princess.

Zena Ramadhani na Elizabeth Chenge, waliifungia pia JKT Queens katika mechi hiyo ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jenerali Isamuhyo hapo juzi.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo, Yanga Princess ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa KMC Complex ilipata ushindi wa mabao 3-0 wakati Ceasiaa pia iliifunga Mashujaa Queens magoli 2-0 sawa na ushindi ambao Gets Program iliupata dhidi ya Mlandizi Queens.

Mabao ya Gets Program katika mchezo huo wa raundi ya 10 yalifungwa na Winifrida Juma na Beatrice Charles.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Yusif Basigi, aliliambia gazeti hili mechi hiyo ilikuwa ngumu kwa sababu walikutana na wachezaji wenye kasi.

Basigi alisema alifanyia kazi mapungufu ya kikosi chake yaliyoonekana katika kipindi cha kwanza na waliporejea dakika 45 za mwisho walikuwa imara.

"Tumekutana na timu nzuri, yenye uwezo na kasi, lakini ubora wa wachezaji wangu ulisaidia kubadilisha matokeo, nashukuru kipindi cha pili tulitawala mchezo," alisema Basigi.

Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itaendelea tena Februari 4, mwaka huu kwa Mashujaa Queens kuwaalika Yanga Princess, Mlandizi kuikabili JKT Queens, Alliance Girls dhidi ya Gets Program huku Bunda Queens itawakaribisha Fountain Gate Princess na Simba Queens itarejea nyumbani kuwaalika Ceasiaa Queens.



Kikosi cha Alliance Girls kikiwa na picha ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Alliance Schools, James Bwire, kabla ya mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Yanga Princess iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi. Marehemu Bwire alifariki hivi karibuni na mazishi yake yalifanyika Jumapili iliyopita mkoani Mara. **PICHA: MTANDAO**

# JKT Tanzania yaihofia Coastal Union

**Na Somoe Ng'itu**

TIMU zimejipanga, hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Ahmad Ally kuelekea mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Coastal United itakayochezwa Februari 7, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid.

Kocha huyo alisema kikosi chake kinaendelea kujipanga kwa sababu anaenda kukutana na Coastal Union iliyoimarika.

Alisema mechi zote za mzunguko wa pili huwa na ushindani kwa sababu timu zimerekebisha makosa na zimeimarisha vikosi kwa kuongeza wachezaji wapya wakati wa dirisha dogo.

"Niseme tu Coastal Union ambayo iko chini ya Mwambusi (Juma), imeimarika, sio ile, tunajiandaa vyema kuikabili, hautakuwa mchezo mwepesi," alisema kocha huyo.

Winga wa timu hiyo, Shiza Kichuya, alisema wachezaji wote wamejipanga kusaka matokeo chanya na wanaamini hilo linawezekana.

"Tuko tayari kwa mechi hiyo, tumefanya maandalizi mazuri, ninaamini kama tutafuata maelekezo vyema, kokote unapata ushindi, tunaenda kupambana ili turudi na pointi tatu muhimu," Shiza alisema.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Bara, JKT Tanzania yenye pointi 19 iko katika nafasi ya nane huku Coastal Union yenye pointi 18 iko kwenye nafasi ya 11, KenGold ya Mbeya inaendelea kuburuza mkia ikiwa na pointi sita kibindoni.

## Morocco: Maandalizi Stars yawe ya kitaifa

INATOKA UKURASA 24

Kocha huyo alisema TFF inahitaji msaada ili kukamilisha programu za kiufundi za timu hiyo ambayo haijawahi kuvuka hatua ya makundi.

Aliongeza kuwafahamu mapema wapinzani wao ni jambo zuri kwa sababu watapata muda mzuri wa kuwafuatilia na kujiandaa kuwakabili.

"Mimi naamini tumepiga hatua kwenye makundi katika kutafuta nafasi ya kushiriki, tumefanya vizuri lakini haitoshi, tunahitaji kupambana zaidi na kuendeleza pale tulipofikia," alisema kocha huyo mwenye asili ya Zanzibar.

Aliongeza katika fainali hizo hakuna timu nyepesi, kila timu iliyofuzu inaweza ikawa tishio, lakini hakuna nchi wanayoihofia.

"'Of course' timu zote ambazo zimefuzu ni tishio, kufika hatua ya fainali za AFCON si jambo la rahisi, la msingi ni kuhakikisha tunajipanga vizuri ili tuwe bora zaidi," Morocco aliongeza.

Kabla ya kushiriki fainali hizo za AFCON, Taifa Stars imekata tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), zitakazofanyika kuanzia Agosti 2 hadi 30, mwaka huu.

Tanzania, Kenya na Uganda ndio wenyeji wa fainali hizo za CHAN, ambazo awali zilitarajiwa kufanyika kuanzia mapema Februari, mwaka huu.

Shirikisho la Soka Afrika (CAF), imezipa nchi hizo tatu wenyeji wa michuano ya CHAN ili kuwapa uzoefu kuelekea Fainali za AFCON za mwaka 2027 ambazo zitaandaliwa na mataifa hayo matatu ya Afrika Mashariki.

Michezo
Alhamisi Januari 30, 2025
Nipashe



United yakaribia kumnasa Dorgu UKURASA 22

# AZIZ KI, MZIZE RASMI SOKONI

●●● Yanga, Wydad kuteta Julai, Simba ikiitisha Tabora United...

**Somoe Ng'itu na Adam Fungamwango**

HATIMA ya wachezaji wawili wa Yanga, Stephanie Aziz Ki na Clement Mzize, ambao wanatakiwa na Wydad AC ya Morocco itajulikana ifikapo Julai Mosi, mwaka huu, imefahamika.

Taarifa za ndani kutoka Yanga, zinasema mabingwa hao watetezi wameiambia Wydad itakuwa tayari kufanya mazungumzo ya kuwauza wachezaji hao muda huo ukifika na si wakati huu.

**Chanzo chetu kilisema uamuzi huo umetokana na Yanga kuwaeleza Waarabu hao inahitaji zaidi mchango wa nyota hao wawili kwa ajili ya vita ya kutetea taji la Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA, ambalo wanayashikilia.**

"Wachezaji wote wawili ni muhimu katika kufikia mafanikio ya klabu yetu, hatuwezi kukubali kuwauza kwa sasa, tutakuwa tayari kufanya mazungumzo ya kuwauza kuanzia Julai Mosi, 2025, kama Wydad mtakuwa bado mnahitaji huduma yao," ilisema sehemu ya barua ya Yanga kwenda kwa Waarabu hao.

Mbali na Wydad, pia klabu mbili zinazoshiriki Ligi Kuu ya Afrika Kusini pia zimeonyesha nia ya kuwahitaji nyota hao ili kuimarisha vikosi vyao.

Wakati huo huo, Yanga inaendelea na maandalizi kwa ajili ya kujiandaa kuwakaribisha Kagera Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, aliliambia gazeti hili wameshafunga 'mafaili' kuhusiana na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na sasa hawataki kupoteza mchezo wao wa keshokutwa.

Kamwe alisema Yanga inataka kurejea kwa 'kishindo' katika Ligi Kuu, mahali ambapo hawana mpinzani ingawa baadhi ya mechi huwa ngumu na yenye ushindani.

"Tunakwenda kucheza mechi muhimu, mechi yetu ya kwanza baada ya kutoka katika michezo ya kimataifa, tumekuwa tukiwaambia wanachama na mashabiki wetu tumetoka kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, tumeumia sana, lakini tutaumia zaidi kama tutakosa kutwaa ubingwa wa Ligi KuuTanzania Bara.

Tunataka tuendeleze rekodi yetu ya kushinda mechi zetu za Ligi Kuu kwa asilimia 100, tangu ujio wa Ramovic (Sead), tumeshinda kwa idadi kubwa ya mabao, hicho ndicho kitakwenda kuwakuta Kagera Sugar," alisema Kamwe.

INAENDELEA UK. 23


Mzize

## Morocco: Maandalizi Stars yawe ya kitaifa

**Na Faustine Feliciane**

ILI kuhakikisha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inafanya vizuri katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), maandalizi yake yawe ni 'jambo' la kitaifa na si kuacha jukumu hilo kwa Serikali na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), imeelezwa.

Katika fainali hizo zitakazofanyika kuanzia Desemba 21, mwaka huu hadi Januari 18, mwakani nchini Morocco, Taifa Stars imepangwa Kundi C pamoja na Uganda (Cranes),Tunisia na Nigeria.

Stars itatupa karata yake ya kwanza Desemba 23, mwaka huu kwa kuivaa Nigeria halafu Desemba 27 itakutana na 'majirani' zake Uganda na itamaliza mechi za hatua ya makundi Desemba 30 kwa kupambana na Tunisia kwenye Uwanja wa Prince Moulay ulioko jijini, Rabat.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Hemed Suleiman 'Morocco' amesema ili kuweka rekodi ya kufanya vyema katika fainali hizo, maandalizi ya timu hiyo yanapaswa kuwa ni jukumu la kitaifa.

Morocco kipindi cha miezi 11 iliyobakia kabla ya kufanyika kwa fainali hizo, matokeo chanya yanaweza kupatikana kama tutaongeza ushirikiano kuanzia hatua ya kwanza.

"Hili jambo si la mwalimu au benchi la ufundi, ni suala la kitaifa hasa pale katika uwezeshwaji wa kutekeleza mipango ya mwalimu, sisi kama benchi la ufundi tutakuja na programu yetu na naamini ikifuatwa vyema tutafanya vizuri kwenye fainali hizi," alisema Morocco.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >